epaper.ippmedia.com
MIAKA 30 Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

Jumapili Januari 12, 2025 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
www.ippmedia.com 0677 020 710
ISSN 0856 • No. 0581919
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA WA 3

**TLS** yaingilia kati sakata la kukamatwa kwa Dk. Slaa

UKURASA WA 3

**Walimu** 201,707 kufanyiwa usaili kujaza nafasi za wazi 14,648



UKURASA WA 7

KONA YA AFYA

**Ijue** homa ya ini na madhara yake kiafya



**Lewandowski: Barca inatakiwa ijiboreshe**

UKURASA 21

## Neema ya Rais Samia yanukia mikoa ya kusini

UKURASA 2



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe (kulia), akiteta jambo na Makamu wake, Tundu Lissu, wakati wa kikao cha Kamati Kuu ya chama hicho, Dar es Salaam jana. **PICHA: RESTUTA JAMES**

## Wiki ya presha kupanda, kushuka CHADEMA

UKURASA 2

RIPOTI MAALUM

# Utapishaji maji vyoo unavyoweka rehani maisha ya wananchi

UKURASA 4



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akitia saini kwenye bango maalum waliloandaliwa viongozi, baada ya kushuhudia Tamasha la Kahawa Afrika, lililolenga kuhamasisha uongezaji thamani katika mazao yanayolimwa Afrika, likiwemo zao hilo, tukio liliondoa sambamba na Mkutano Maalum wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika kuhusu Mpango wa Maendeleo ya Kilimo Afrika, jijini Kampala Uganda jana, akimwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan. Wengine ni pamoja na Rais wa Uganda, Yoweri Museveni na Rais wa Kenya, William Ruto. **PICHA: OWM**

## HERI YA MAPINDUZI

*LEO ni Mapinduzi ya Zanzibar. Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na wafanyakazi wa The Guardian Limited (TGL), wachapishaji wa magazeti ya The Guardian, Nipashe na Nipashe Jumapili, wanawatakia Watanzania wote Heri ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.*

MICHEZO SIMBA, YANGA NI ZAIDI YA VITA CAF UK.24 MAONI, UK.6

## Neema ya Rais Samia yanukia mikoa ya kusini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Ujenzi, Abdallah Ulega, ametangaza kuwa serikali imetenga zaidi ya Sh. bilioni 114 kukarabati barabara za mikoa ya Kusini zilizoharibiwa na mvua ya El- Nino huku akiagiza taa za kutosha kuwekwa kwenye barabara kuu kuelekea mikoa ya Kusini.

Akizungumza katika maeneo tofauti wakati wa ziara yake mkoani Lindi juzi na jana, Ulega alisema kiasi hicho cha fedha kilichotengwa kwa mkoa wa Lindi ndicho kikubwa zaidi kutengwa kuliko mkoa mwingine wowote hapa nchini.

" Ndugu zangu wa Lindi, nimekuja kukagua barabara zetu baada ya matatizo ya mvua za El Nino na hiki kimbunga cha Hidaya. Rais (Samia Suluhu Hassan) ameniagiza nije huku kuangalia hali na kuwapa pole kwa changamoto mnazopitia.

"Kwa mapenzi yake makubwa kwenu na kwa Watanzania kwa ujumla wake, Rais Samia ameagiza tutumie zaidi ya shilingi bilioni 114 kwa ajili ya kurekebisha barabara na madaraja yaliyoharibiwa na kutengengeza njia za kuchepusha," alisema Ulega wakati akiwa eneo la Somanga.

Mvua ya El Nino iliyonyesha nchini mwishoni mwa mwaka jana, ilifuatia msimu wa mvua za masika zilizosababisha uharibifu mkubwa wa miundombinu katika maeneo tofauti nchini, ingawa mikoa ya Kusini iliathirika zaidi.

Katika ziara yake hiyo, Ulega alijionea uharibifu uliosababishwa na mvua hizo na pia juhudi za wakandarasi wanaojenga barabara hizo – wakiwamo wakandarasi wazalendo.

Baadhi ya makandarasi walionyesha kuwa na kasi ya utekelezaji wa ukarabati, wakiwa wamefikia lengo miezi miwili kabla ya wakati waliokuwa wamepewa.

Katika hatua nyingine, Ulega ameagiza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) kuanza kuweka taa katika barabara kuu inayoelekea mikoa ya Kusini ili kukuza shughuli za kiuchumi katika maeneo inakopita.

Waziri huyo ambaye sasa ameanza kujipambanua kwa kaulimbiu yake ya usiku na mchana, alisema sera za Rais Samia ni za kukuza uchumi na kuwa maeneo ambako kuna giza ni vigumu kwa uchumi kukua.

"TANROADS naomba taa zianze kuwaka kwenye barabara hii ya kuja Kusini mwa Tanzania. Haya ni maelekezo ya Rais wetu na kazi yenu ni kuhakikisha mnatekeleza agizo hilo kwa kufanya kazi usiku na mchana," alisema.

Mbali na kukagua maendeleo ya ukarabati wa miundombinu, Ulega pia anatumia ziara hii kueleza mafanikio kadhaa yaliyopatikana kwenye eneo la ujenzi kwenye miaka mitatu ya uongozi wa Rais Samia.




Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega (kulia), akisikiliza maelezo kuhusu maendeleo ya ukarabati wa barabara zilizoharibiwa na mvua kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Mohamed Moyo, katika maeneo tofauti ya wilaya yake na ya Ruangwa. Ulega yuko mkoani Lindi kwa ajili ya ukaguzi wa barabara hizo. **PICHA: WIZARA YA UJENZI**

# Wiki ya presha kupanda, presha kushuka CHADEMA

**Na Restuta James**

NI wiki ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA). Hii ni kwa sababu ni wiki ya kupata viongozi waandamizi wa chama hicho kikuu cha upinzani nchini.

Aidha, uchaguzi wa wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti na Makamu wake ngazi ya taifa ni Jumanne ijayo wakati hatima ya Katibu Mkuu, John Mnyika na Manaibu wake, itajulikana Januari 22, mwaka huu.

Juzi na jana, Kamati Kuu ya chama hicho imekutana Dar es Salaam, kuteua wagombea wa nafasi mbalimbali kwenye mabaraza ya chama hicho ya Vijana (BAVICHA), Wanawake (BAWACHA) na Wazee (BAZECHA), kati ya 303 waliojitokeza.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema, alisema kwa siku ya jana, kamati hiyo imefanya uteuzi wa wagombea wa nafasi mbalimbali za BAWACHA Taifa.

Alisema wagombea 93 wamejitosa kuwania nafasi ndani ya baraza hilo la wanawake, BAVICHA (69) na BAZECHA (85).

Alisema idadi kubwa ya wagombea waliojitokeza ndio imesababisha Kamati Kuu, kutumia siku mbili kuwahoji na kuteua.

"Kamati Kuu inaendelea na vikao vya uchujaji na uteuzi wa wagombea ambayo ilianza jana (juzi), leo (jana), tunafanya usaili wa BAWACHA Taifa," alisema.

Mrema alisema mchakato wa uchaguzi ndani ya mabaraza hayo unaendelea vizuri na kwamba leo Kamati ya Utendaji ya BAVICHA itakutana kwenye kikao cha kuandaa Mkutano Mkuu utakaofanyika kesho Jumatatu katika ukumbi wa Ubungo Plaza, Dar es Salaam.

"Uchaguzi wa Baraza la Wazee nao utafanyika keshokutwa. Uchaguzi wa Baraza la Wanawake utafanyika tarehe 16 (Alhamisi). Baada ya hapo tutakuwa na vikao vingine vya kuhoji na kuchuja wagombea wa nafasi za chama Taifa (Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti)," alisema.

Alisema kwenye uchaguzi wa mabaraza watapatikana wajumbe wapya wa Kamati Kuu, akitoa mfano wa BAVICHA ambako Mwenyekiti wake wa sasa, John Pambalu, amemaliza muda wake na hana sifa za kugombea tena.

Kutokana na hilo, Kamati Kuu itakayowateua Mbowe na Lissu, itakuwa na sura mpya.

"Ikumbukwe kwamba watakaochaguliwa kuwa Wenyeviti kwenye mabaraza wanakuwa wajumbe wa Kamati Kuu. Kwa hiyo wako wajumbe wapya watakaoingia. Mfano ni Mwenyekiti mpya wa BAVICHA, atashiriki kuteua wagombea wa nafasi ya chama Taifa," alisema.

Alisema baada ya uteuzi wa wagombea wa Mwenyekiti na Makamu wake, majina yatapelekwa Baraza Kuu na kisha Mkutano Mkuu Januari 21, 2025.

Mrema alisema baada ya uchaguzi mkuu, Baraza Kuu la CHADEMA litakutana tena Januari 22, kwa ajili ya kuteua Katibu Mkuu, Manaibu wake na wajumbe nane wa Kamati Kuu.

Kwa siku hizo mbili, kikao cha Kamati Kuu kinaongozwa na Mbowe anayegombea kutetea nafasi yake kwa mhula mwingine, akisaidiana na Lissu ambaye amejitosa kutaka kumng'oa kwenye kiti hicho. Mgombea mwingine aliyejitosa kwenye Uenyekiti ni Charles Odero.

Kikao hicho kimehudhuriwa pia na wagombea wa nafasi ya Makamu Mwenyekiti wanaowania kurithi nafasi ya Lissu, Ezekia Wenje na John Heche, ambaye alitangaza kuwa upande wa Lissu.

**WAGOMBEA BAZECHA**

Januari 07, mwaka huu Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, kupitia mkutano wake na waandishi wa habari, alisema wagombea katika nafasi ya uenyekiti wa Bazecha Taifa, ni Hashim Juma Issa, John Mwambigija, Hugo Kimaryo, Mwecha Tiba na Suzan Lyimo.

Katika nafasi ya Katibu Mkuu, wagombea wako watatu ambao ni Dk. Leonard Mao, Hellen Mayanza na Kasmiri Mabina, wakati katika nafasi ya naibu katibu mkuu (Bara), waliojitokeza ni Hamid Mfaligundi na Omary Mkama na kwa upande wa naibu katibu mkuu (Zanzibar) ni Rajab Hamis Bakari na nafasi ya mweka hazina ni Florence Kasilima.

**BAVICHA**

Kwa upande wa Bavicha, waliojitokeza kugombea uenyekiti ni Deogratius Mahinyila, Hamis Masoud na Shija Shibesi.

Kwa nafasi ya makamu mwenyekiti (Bara), wagombea ni Vitus Nkuna, Baraka Charles, Necto Kitiga, Juma Ng'itu, Nice Sumari na Mkola Masoud.

Nafasi ya makamu mwenyekiti (Zanzibar), wagombea ni Abdallah Haji na Kassim Abdallah. Katibu mkuu ni Benjamin Nteje, Idrisa Kassim, Ambokile Mwangosi, Dua Lwamzito na Sheila Mchamba.

Waliojitokeza nafasi ya naibu katibu mkuu (Bara) ni Emmanuel Kasturi, Mussa Bashar na Levin Mbughi, wakati nafasi ya naibu katibu mkuu (Zanzibar) ni Awena Nassoro na Said Abdulla Khamis. Nafasi ya mratibu wa uhamasishaji wamejitokeza wagombea wawili, Felius Kinimi na Dedan Wangwe.

Kwa upande wa Mweka hazina wagombea ni Michael Materu, Badi Ibrahim, na Ramna Abdallah.

HABARI KITAIFA

# Walimu 201,707 kufanyiwa usaili kujaza nafasi 14,648

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WALIMU 201,707 wanatarajiwa kufanyiwa usaili kuanzia Januari 14 hadi Februari 24, mwaka huu, kwa ajili ya kujaza nafasi 14,648 zilizotangazwa na serikali ili kupunguza uhaba wa watumishi wa kada hiyo nchini.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu usaili huo.

"Kuanzia tarehe 14 Januari hadi tarehe 24 Februari, 2025, usaili wa kada za ualimu utaendeshwa na Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais (UTUMISHI).

Pia itahusisha Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Afya, Tume ya Utumishi wa Walimu, Ofisi za Wakuu wa Mikoa yote na wataalamu mbalimbali kutoka katika Taasisi za Umma, alisema

Simbachawene alisema usaili huo una lengo la kujaza nafasi 14,648, zilizotolewa na Rais kwa lengo la kupunguza uhaba wa walimu nchini.

"Ninapenda kuchukua nafasi hii kuwasihi sana wale wote walioitwa kwenye usaili wajiandae vyema kwa usaili huo kwani nafasi hizi ni za ushindani.

"Vilevile, kulingana na mahitaji yetu ya elimu kwa sasa, tutaajiri wataalamu wa fani za Amali. Hivyo, nawasihi sana wale wote watakaopata nafasi ya kuajiriwa, wawe tayari kujiendeleza ili kuweza kukidhi matakwa ya ajira zao katika Utumishi wa Umma," alisisitiza.

Aidha, alisema usaili huo wa kada za ualimu utafanyika katika Mkoa ambao kila msailiwa anaishi lengo ni kuwapunguzia gharama za kusafiri na mambo mengine.

"Sekretarieti ya Ajira ilitoa matangazo kumtaka kila msailiwa kuhuisha taarifa zake katika akaunti yake ya 'Ajira Portal' sehemu iliyoandikwa 'current physical adress' kwani ndipo tumewapangia vituo vya usaili kulingana na anuani walizojaza," alisema.

Pia aliwasihi waombaji wote kuhakikisha kila mmoja anakwenda katika kituo ambacho amepangiwa kwa ajili ya usaili kwani mahitaji yake ya msingi yapo huko.

Vile vile, alisema usaili wa awali wa kuandika (Mchujo) kwa kada za ualimu utafanyika kwa njia ya kuandika kwa mkono kwa kada zote na ngazi zote za elimu.

"Ninapenda kuwakumbusha wale wote watakaokwenda kwenye usaili wahakikishe wanabeba vyeti vyao halisi kikiwemo cheti cha taaluma na cheti cha kuzaliwa,"alisema.

# TLS yaingilia kati sakata kukamatwa Dk. Slaa

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Wanasheria Tanganyika (TLS), kimevitaka vyombo vya dola kutofautisha kati ya majibizano ya kisiasa na makosa ya kijinai ili kutenda haki kwa watuhumiwa.

Rais wa Chama hicho, Wakili Boniface Mwabukusi, amesema kesho atakwenda kumwakilisha Balozi na Katibu Mkuu Mstaafu wa CHADEMA, Dk. Wilbrod Slaa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Dk. Slaa alikamatwa na Polisi juzi asubuhi na saa 8:00 mchana alipandishwa katika mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kujibu shtaka la kusambaza taarifa za uongo kupitia mtandao wa X.

Kupitia mtandao wa kijamii wa X jana, Wakili Mwabukusi alisema tuhuma zinazotokana na masuala ya kisiasa ni vyema zikashughulikiwa kwa misingi ya kisiasa, badala ya kuzihamishia kwenye mfumo wa jinai.

Alisema mfumo wa haki jinai haupaswi kutumika kama chombo cha visasi, kukomoa, au kunyima watu haki zao za kikatiba bali msingi wa kuwarekebisha wahalifu kwa haki na uwazi.

"Katika mazingira ya ukosoaji wa kisiasa, ni muhimu kuweka mipaka kati ya haki za kibinafsi na makosa ya jinai," alisema.

Alisema mambo ya kibinafsi yashughulikiwe kwa njia za kibinafsi na si kwa kutumia nguvu ya dola isivyo halali.

"Tutaimarisha na kulinda utawala wa sheria kwa kujitokeza mahakamani mara zote, bila woga, tukisimama kidete kwa ajili ya ukweli, katiba, na sheria," alisema.

Mwabukusi alisema matokeo ya kesi si jambo kuu, kilicho cha msingi ni kulinda misingi ya haki na kuhakikisha sheria zinatekelezwa kwa uadilifu.

**ILIVYOKUWA MAHAKAMANI**

Akimsomea Dk Slaa Shtaka, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Beda Nyaki , Wakili wa Serikali, Clemence alidai kuwa mshtakiwa alitenda kosa hilo Januari 9, mwaka huu, ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikielezwa kupitia jukwaa la mtandao wa kijamii wa X katika akaunti ya Maria Sarungi @MariaSTsehai.

Alidai kuwa aliandika ujumbe uliosomeka: "Wakubwa wametafutana, nikisema wakubwa namaanisha Mwamba na Samia, na wala hatuna maneno ya kumung'unya... na kimsingi wamekubaliana Suluhu Samia amekubali atatoa pesa, Suluhu Samia amekubali ataongeza nguvu ya pesa ni dhahiri atatoa pesa hizo ni hela za Watanzania wanazichezea Samia na watu wake."

Alidai kuwa mtuhumiwa katenda kosa hilo chini ya kifungu cha 16 cha Sheria ya Makosa ya Mtandao namba 14 ya Mwaka 2015.

Mawakili wa utetezi waliofika mahakamani hapo juzi wakiongozwa na Peter Madeleka walieleza kushangazwa na kitendo cha mawakili wa serikali kutoa kiapo cha kupinga Dk. Slaa kupewa dhamana bila kuwashirikisha na kukubaliana kwa pamoja.

Akizungumzia suala hilo, Wakili Madeleka alisema dhamana ni haki ya mtu huwezi mnyima mtu kwa kuwa alitoa kauli ya jumla, kwa kuwa sheria ni uwanja unaohitaji uandilifu tofauti na walivyofanya mawakili wa serikali.

"Kiapo hicho kilikuwa hakijawasilishwa kwa mawakili wa upande wa pili (utetezi) lakini pia wameeleza kuwa kwa kuwa upelelezi haujakamilika wameomba iahirishwe na ndugu Slaa asipewe dhamana kwa sababu ya usalama wake," alisema

Madeleka alisema walipopata taarifa za kukamatwa kwa Dk. Slaa juzi asubuhi walifuatilia katika vituo vya Polisi vya Mbweni, Osterbay na Kituo Kikuu bila mafanikio.

Alisema baadaye walikutana na Kamanda wa Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, aliyewaeleza makosa yanayomkabili na kuwa alipelekwa katika Mahakama ya Kisutu.



Wananchi wakipita jirani na lundo la takataka lililotelekezwa bila ya kuzolewa kwa muda mrefu, kando ya barabara ya Kilwa, eneo la Mbagala Zakhem, Dar es Salaam jana, zinazosababisha usumbufu kwa wapita njia na kuhatarisha afya za wafanyabiashara wa eneo hilo. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# DC, bodaboda walioandamana na kufunga barabara wakaa mezani

**Na Remmy Moka**

BAADA ya maandamano ya waendesha bodaboda na bajaji mkoani Kigoma kutikisa huku wengi wao wakitiwa mikononi mwa polisi, Mkuu wa Wilaya ya Kigoma, Dk. Rashid Chuachua, amewaita kusikiliza kero zao huku akiwataka kufuata taratibu zote za kisheria.

Akizungumza na madereva hao, Dk. Chuachua alisema serikali na kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya hawakuridhishwa na vurugu hizo.

Alisema vurugu hizo za waendesha bodaboda na bajaji kufunga barabara hawategemei kuona tena zikijitokeza kwa kuwa hazileti taswira nzuri kwa mkoa na taifa kwa ujumla.

Dk. Chuachua alisema tayari wamefanya mazungumzo na viongozi wao wa vituo vya bodaboda ili kuhakikisha wanaweka mazingira ya hali ya utulivu baina ya wasafirishaji wa vyombo vya moto na serikali.

Kadhalika, aliwataka madereva hao kuhakikisha wanafanya mchakato wakupata leseni ili kuondoa malalamiko yasiyo ya msingi pamoja na kutii sheria bila shuruti kwa kuwa serikali imepokea malalamiko yao na imeahidi kuyafanyia kazi.

"Kuhakikisha mnakidhi matakwa ya vyombo vya usalama barabarani. Hakikisheni mnaenda katika vyuo vya mafunzo ya udereva VETA ili muwe na uhalali wa kupata leseni na kuacha mivutano na Jeshi la Polisi," alisema.

Dk. Chuachua alisema ni vyema wakafanya shughuli zao kwa usalama zaidi ili kulinda uhai wao pamoja na watumiaji wengine wa barabara. Alisema kwa kipindi cha 2023 ajali za pikipiki zilitokea 42 huku waendesha bodaboda waliofariki ni 12 na watembea kwa miguu 17 huku 2024 zikitokea ajali 50 za bodaboda wakifariki Dunia, waendesha bodaboda 22 na watembea kwa miguu 16.

Nao baadhi ya waendesha bodaboda na bajaji, walisema wamepokea maelekezo hayo lakini wakiliomba Jeshi la Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani kuwa na utaratibu mzuri wa ukamataji kwa waendesha vyombo vya moto ili kuondoa migogoro baina yao pamoja na sintofahamu hasa wanapokuwa wakikamata huku wamevalia kiraia

Mmoja wa waendesha bodaboda hao, Ramadhani Musa, alisema wanategemea serikali itahakikisha wanawawekea hali nzuri ya shughuli zao na watatii sheria bila shuruti ikiwamo kwa wale ambao hawana leseni watafanya utaratibu wa kupata leseni za udereva.

RIPOTI MAALUM

# Utapishaji vyoo waweka rehani maisha ya watu

**Na Vitus Audax,** MWANZA

"SISI wenyewe hatuko salama lakini ndiyo kazi yetu". Ni sauti ya Samson Makuri, msaidizi wa Chacha Marwa watapisha vyoo kutoka Kata ya Mabatini jijini Mwanza.

Ni katika mtaa wa Mabatini Kusini, eneo la milimani kando kidogo na Zahanati ya Mabatini, hali ya wakazi wa maeneo haya kwa mwonekano na uchakavu wa majengo inadhihirisha kuwa ni duni.

Majira ya saa 4:00 usiku, watoto kwa wakubwa wanaendelea na shughuli mbalimbali ikiwamo kumalizia mapishi kwa ajili ya mlo wa jioni. Sauti za redio zinazosikika kwa kupokezana katika eneo hili, zinatawaliwa na simulizi tofauti zinazoashiria ni muda wa mapumziko.

Licha ya sauti za redio hizo kulazimu watu wakalale, mwandishi wa ripoti hii anashuhudia watu wawili ambao kwao ndio kumekucha, wakiendelea na kazi ngumu kwa kuitazama lakini ni rahisi na iliyozoeleka kwa mujibu wa maelezo yao.

Huu ni utapishaji wa vyoo kwa njia za kienyeji wakati wa kiangazi, utaratibu wanaouita kuwa wa kawaida kwa wakazi waishio milimani jijini hapa.

Walichojiandaa nacho wawili hao ambao hali yao ni ya ulevi wakati wote ni mafuta ya taa pekee pamoja na vifaa duni kama vile ndoo, sepetu (koleo) na jembe. Hakuna glovu wala vifaa maalum vya kujistiri dhidi ya uchafu huo.

Njia hii ambayo si salama, si tu kwao bali hata kwa wananchi wanaoishi maeneo husika, kutokana na hatari ya magonjwa ya mlipuko hususani inaponyesha mvua. Kadhalika ni hali inayosababisha uchafuzi wa mazingira pamoja na hewa chafu wakati wa utapishaji kwa wakazi wa maeneo ya jirani.

Wakati wa kiangazi, wananchi waishio katika baadhi ya maeneo ya milimani, hutumia watapisha vyoo hawa, maarufu kama 'topazi' ambao huzibua vyoo na kuhamishia uchafu katika shimo mbadala hali inayoibua pia harufu mbaya katika makazi ya watu. Hali hiyo pia husababisha uchafuzi wa mazingira kwa eneo husika.



Chacha Marwa (51) (aliyesimama ndani ya chemba ya choo) ambaye ni Mkazi wa Mabatini na Mtapishaji wa vyoo katika maeneo mbalimbali jijini Mwanza kupitia kikundi chao maarufu kama Tobazi, akitoa majitaka ndani ya choo huku akisaidiwa na mwenzake, Samson Makuri. **PICHA: VITUS AUDAX**

**SIMULIZI MTAPISHAJI**

Chacha Nyechi (51), Mkazi wa Mabatini Kusini na mtapishaji wa vyoo, anasema alianza kazi hiyo mwaka 1988 na kuwa kazi hiyo amekuwa akiwafanyia wananchi wa maeneo ya milimani hasa wale wenye hali duni na wanaojipatia riziki kwa kufanya shughuli tofauti zisizo rasmi.

Anasema gharama za kufanya kazi hiyo ni kati ya Sh.70,000 hadi 100,000 kulingana na ukubwa wa choo. Anasema kazi hiyo inahitaji watu wawili hadi watatu kuifanya kutokana na ugumu wake na kuhakikisha wanaifanya kwa ufanisi.

"Tulitumia hali ya kukosekana kwa miundombinu ya uzoaji wa taka hizi kama fursa baada ya kuona watu wanateseka. Lakini kazi hii tunaifanya katika mazingira magumu bila kuwa na glovu wala vifaa maalumu vya kufanyia kazi hii, hali inayosababisha tunakuwa hatarini," anasema.

Pia anasema wakati wa kufanya kazi hiyo, hujipaka mafuta ya taa kisha mengine humwaga kwenye choo ili kupunguza harufu mbaya wakiwa kazini na kuua wadudu ili waendelee na kazi bila tatizo.

"Tunaomba serikali itusaidie kupata vifaa ili kufanya kazi hii kwa weledi na kuzikinga afya zetu dhidi ya magonjwa," anasema Chacha ambaye hata hivyo hali yake ni ya ulevi wakati wote.

Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Usafi na Mazingira wa Jiji la Mwanza, Desderius Polle, anasema vikundi hivyo vinatambuliwa na serikali na wamekuwa wakipewa mafunzo ya kuhakikisha wanazibua kwenye chemba za watu na kuingiza kwenye mfumo wa maji machafu ili kutokuchafua mazingira na vyanzo vya maji.

Hata hivyo, hatua hiyo ni tofauti na kinachoendelea mtaani kwa kuwa utapishaji unafanyika katika eneo moja na shimo kuchimbwa pembeni na taka hizo zinafukiwa, hali inayoweza kusababisha mlipuko wa magonjwa pindi mvua ikinyesha.

Takwimu kutoka Halmashauri ya Jiji la Mwanza zinaonesha kuwa zaidi ya watu 860 katika jiji hilo lenye wakazi takriban 426,154 waliugua magonjwa ya mlipuko yakiwamo kuhara na homa ya matumbo katika kipindi cha miezi sita kuanzia Aprili mpaka Septemba, 2024.

Mlipuko wa kipindupindu uliotokea nchini mwanzoni mwa mwaka 2024, Mwanza iliripoti kifo kimoja na wagonjwa 112 kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza.

Kadhalika, ripoti ya Wizara ya Afya ya Mashindano ya Afya na Usafi wa Mazingira ya mwaka 2023, kipengele cha Majiji na Manispaa iliyotolewa Mei 10, 2024, inaonesha kuwa Mwanza ilishika nafasi ya mwisho kwa kupata asilimia 57 na alama 71 kati 124. Tanga ikiibuka ya kwanza kwa asilimia 84 likifuatiwa na Mbeya 78, Arusha 77, Dar es Salaam 66 na Dodoma 60. Hali hii inaonesha ni kwa namna gani bado kuna haja ya juhudi kuongezwa katika kudhibiti uchafuzi wa aina zote.

**HALI WAKATI WA MVUA**

Kutokana na jiografia ya jiji la Mwanza, inaelezwa kuwa asilimia 70 ya wakazi wake wanaishi milimani ambako ni vigumu kujenga vyoo vya shimo refu hali inayosababisha kutengenezwa mashimo mafupi na kuachiwa mfumo wa kufungulia uchafu pindi mvua inaponyesha maarufu kama 'tegesha'.

Bahati Ally (50), Mkazi wa Mtaa wa Nyerere 'A', Kata ya Mabatini anasema kwa miaka yote aliyoishi katika eneo hilo wamekuwa wakishuhudia utiririshaji wa kinyesi kutoka kwa wakazi wa maeneo ya juu wakati wa mvua lakini tatizo ni jinsi ya kutambua ni kinanani wanaofanya hivyo.

"Kwa milimani unakuta mtu anapata sehemu ya kujenga choo lakini hana pa kuweka shimo hali inayosababisha mara nyingi wanategeshea kipindi cha mvua na kumwaga kinyesi.

"Madhara tunayokutana nayo mara nyingi ni pamoja na maradhi hasa kwa watoto, kipindupindu cha mara kwa mara maambukizi kwa njia ya mkojo (UTI) na uchafuzi wa mazingira," anasema Bahati.

Sehemu ya madhara anayoyataja Bahati, yanathibitishwa kwenye maelezo ya Ofisa Afya wa Jiji la Mwanza, Audiphace Sabbo, anayeitaja kata hiyo kuwa miongoni mwa maeneo kata korofi kwa magonjwa ya kuhara akidhihirisha kuwa hali hiyo inaonesha wananchi wanakula kinyesi.

Anasema kuna haja serikali kutazama suala hilo upya na kuja na mikakati bora ya kutokomeza uchafuzi huo ili kuwalinda wananchi dhidi ya maradhi ya mlipuko hasa katika kipindi cha mvua.

**JAMBO LA KAWAIDA**

Mkazi wa Sahara Juu, Kata ya Pamba, Juma Abdallah anasema utaratibu huo umekuwa wa muda mrefu kwani wamekuwa wakikutana na vinyesi katika mazingira kutokana na watu kufungua chemba za vyoo na kutiririsha uchafu.

"Mvua ikifululiza lazima ushuhudie hiyo hali na mara nyingi nadhani chanzo ni kwamba wanakwepa gharama za kutapisha vyoo vyao. Ni vyema serikali iingilie kati hili suala kwa kuboresha miundombinu ili magari yafike juu hasa milimani," anasema Abdallah.

Aidha anasema adha ambazo

**INAENDELEA UK. 8**

# Watakiwa kufuata vitambulisho NIDA

**Na Halfani Chusi**

NAIBU Waziri wa Mambo ya Ndani, Daniel Sillo, amewataka wananchi ambao hawajapata vitambulisho vya uraia wakavichukue sehemu walikojisajili.

Sillo alitoa rai hiyo juzi jijini Dar es Salaam baada ya kufanya ziara katika sehemu zinazochakata vitambulisho hivyo.

Alisema kitendo cha serikali kutoa Sh bilioni 42.5 kwa ajili ya kuhakikisha waliopata namba wanapatiwa vitambulisho vya taifa kimeleta matokeo chanya.

"Vitambulisho 20,000,000 tayari vimeshasambazwa kwa wananchi, ambao bado hawajachukua watatumiwa meseji kwenye simu zao inayo waonesha mahali kwa kwenda kuchukua kitambulisho na kumaliza kilio chao.

"Nimegundua wapo wanaojisajili zaidi ya mara moja na kwa majina tofauti hali hiyo inawapa tabu wahakiki kwa kuwa vitambulisho hivyo ni kwa ajili ya usalama wa taifa" alionya Sillo huku akisifu utendaji kazi wa NIDA (Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa)," alisema.

Sillo alisema, tayari NIDA imeanza kuifanyia kazi changamoto hiyo kwakuwa hawawezi kutoa vitambulisho bila kujiridhisha au kuwa na taarifa sahihi.

Kadhalika, aliwataka baadhi ya wananchi kuepuka tabia ya kupeleka taarifa za uongo wanapohitaji vitambulisho akisisitiza kufanya hivyo hakutawasaidia.

Mkurugenzi Mkuu wa NIDA, James Kaji, alisema mtu anapofikisha umri wa miaka 18 atembelee kituo cha uandikishaji ili apate kitambulisho kwa sababu kumekuwa na mrundikano wa wahitaji pale nafasi za kazi zinapojitokeza au za chuo.

Alisema kwa sasa wameweka mfumo wa kuwatumia meseji ambapo wanatarajia mpaka mwishoni mwa mwezi huu vitambulisho vyote viwe vimechukuliwa.

Alisema tangu juzi walipoanza kutumia mfumo wa kutuma meseji tayari zaidi ya watu 400,000 siku hiyo kuanzia asubuhi mpaka mchana walipatiwa vitambulisho.

Alisema kutokana na mwitikio huo mpaka kufikia mwisho wa mwezi huu vitambulisho vyote vitakuwa vimechukuliwa.

"Ninapata kesi nyingi kuna walioachishwa kazi kama 600,000 hivi kwa majina feki sasa wanataka kurudi kwaajili ya kutumia majina yao halisi lakini wakiweka alama ya kidole jina linasoma lilelile wamekuwa wengi ni wapiga kelele ninaomba acheni kupiga kelele kwa kuwa hilo ni kosa kisheria kwa sababu walifoji," alisema Kaji.




Mkuu wa Wilaya ya Nzega, mkoani Tabora, Naitapwaki Tukai, akizungumza kuhusu utekelezaji wa watu kufungiwa nishati ya umeme kupitia Wakala wa Nishati Vijijini (REA), kwenye vitongoji, wakati wa mkutano wa hadhara, mjini Nzega, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Adaiwa kumuua mkewe kwa kumchinja

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKAZI wa Kijiji cha Maweni, Kata ya Magara, Babati mkoani Manyara, Shabani Rajabu (60), anadaiwa kumuua mke wake kwa kumchinja shingoni na kumkata mkono katika tukio lililozua simanzi na hasira kwa wakazi wa eneo hilo.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti wa Kitongoji cha Maweni A, Zakaria Serea, mwili wa marehemu ulipatikana ukiwa na majeraha ya kutisha, huku shingo ikiwa imekatwa na majeraha mbalimbali mwilini mwake.

Majirani wa familia hiyo wamelaani vikali tukio hilo, wakieleza kuwa mwanamama huyo alikuwa mtu mwenye tabia ya ulevi yeye na mume wake lakini hawakutarajia kutokea kwa mauaji hayo kwa kuwa mara nyingi walikuwa wakigombana na kupatana.

Hata hivyo, inadaiwa kuwa chanzo cha mauaji hayo ni ulevi na wivu wa kimapenzi.

Jeshi la Polisi lilifika eneo la tukio na kuuchukua mwili wa marehemu na kuupeleka kwenye chumba cha kuhifadhia maiti.

**Wakati huo huo**, mwenyekiti wa kitongoji amewataka wanakitongoji kuepuka kujichukulia sheria mkononi na kutafuta suluhisho la amani kwa migogoro ya kifamilia.

Tukio hili linaongeza idadi ya matukio ya ukatili wa kijinsia mkoani Manyara, hali inayohitaji juhudi za pamoja kati ya jamii, serikali, na mashirika ya kutetea haki za binadamu.

Alipotafutwa na Nipashe kwa njia ya simu kamanda wa polisi mkoani Manyara Ahmed Makarani hakupokea simu.

# Ajali daladala ilivyoua mmoja, kujeruhi wanne

**Na Vitus Audax,** MWANZA

MWANAMKE mmoja ambaye jina lake halikutambulika mara moja, anayedhaniwa kuwa na umri kati ya miaka 20 hadi 25, amefariki dunia katika ajali iliyohusisha daladala kugonga magari matatu.

Akithibitisha kutokea kwa ajali hiyo jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Naibu Kamishna (DCP) Wilibroad Mutafungwa, alisema ilitokea juzi majira ya saa 1:00 asubuhi katika eneo la Iseni, Kata ya Butimba, wilaya ya Nyamagana.

Alisema ajali ilitokea katika barabara ya Kenyatta ambako gari lenye namba za usajili T. 207 DQZ aina ya Toyota Coster likitokea Nyegezi kwenda Mwanza mjini, liligonga gari yenye namba za usajili T. 876 DDA Toyota IST.

Kamanda Mutafungwa alisema gari hilo aina ya IST lililokuwa likiendeshwa na Costantinius Mabele (32), Mfanyabiashara na Mkazi wa Mkolani, liligonga gari lingine lenye namba za usajili T. 571 DND aina ya Toyota Hiace lililokuwa likitokea Mwanza mjini kwenda Nyegezi.

"Katika ajali hiyo mtu mmoja jinsia ya kike anayekadiriwa kuwa na umri wa miaka 20 hadi 25 amefariki dunia na watu wanne wamejeruhiwa," alisema DCP Mutafungwa.

Kamanda Mutafungwa aliwataja majeruhi katika ajali hiyo kuwa ni Maua Rashid (30), Mkazi wa Buhongwa, Fabiani Ndalo (50), Hadija Mussa (24), mkazi wa Kiloleli na David Mussa (27), Mkazi wa Kiseke 'A'.

Alisema wamepelekwa katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando na kuwa chanzo cha ajali hiyo ni uzembe wa dereva wa gari yenye namba za usajili T. 207 DQZ kuyapita magari mengine sehemu isiyoruhusiwa bila kuchukua tahadhari.

Pia alisema baada ya ajali hiyo dereva wa gari hilo alitokomea kusikojulikana na kuwa Jeshi hilo limeanza msako wa kumtafuta dereva huyo ili aweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

"Tunawakumbusha watumiaji wa barabara kufuata sheria, kanuni na taratibu za usalama barabarani kwani hatutasita kuchukua hatua kali kwa watakaobainika kuvunja sheria hizo," alisema DCP Mutafungwa.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mapinduzi ya Zanzibar yameleta mengi mazuri miaka 61, yaenziwe kwa vitendo

**LEO** ni miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wananchi wa Zanzibar na Watanzania kwa ujumla, wanakumbuka Mapinduzi hayo matukufu yaliyoung'oa utawala wa Sultan wa Oman aliyetawala visiwa hivyo na kuwezesha wananchi kujitawala kutoka katika makucha ya wakoloni.

Januari 12, 1964 wananchi wa Zanzibar baada ya kuchoshwa na kufanyiwa ghiliba za kila aina wakati wa harakati za ukombozi na hatimaye kupata uhuru kamili, waliamua kwa nguvu moja kwa kutumia marungu na mapanga, kujikomboa kutoka katika vifungo hivyo vya kutawaliwa na wageni.

Mapinduzi hayo yanakumbusha historia ya visiwa vya Zanzibar, yaani Unguja na Pemba, katika kujikomboa kwao kutoka katika kukandamizwa na kuwa wanyonge ndani ya taifa lao. Kazi hiyo yenye kutukuka, iliyofanikisha kufikiwa kwa azma hiyo, ilifanywa na wanyonge-wakulima, wavuvi na wakwezi wakiongozwa na viongozi wao chini ya Hayati Sheikh Abeid Amani Karume, Rais wa Kwanza wa Zanzibar.

Kabla ya Mapinduzi hayo matukufu, wananchi hao walinyanyaswa na kubaguliwa katika mambo mbalimbali kama vile elimu, afya na huduma. Kulikuwa na matabaka katika utoaji wa huduma na wazawa ambao ni Waafrika na wenyeji halisi wa Zanzibar, walitengwa na kuonekana kuwa ni daraja duni. Hiyo ndiyo moja ya sababu zilizofanya wazawa wajikusanye na hatimaye kufanya mapinduzi hayo matukufu yaliyoleta uhuru ndani ya visiwa hivyo.

Baada ya Mapinduzi hayo, Mzee Karume aliondoa matabaka na ubaguzi uliokuwa umetamalaki na kuweka bayana kuwa watu wote ni sawa. Kwa maana hiyo, mapinduzi hayo jambo la kwanza lililofanikiwa ni kuondoa ubaguzi baina ya wazungu, waasia na waafrika ndiyo maana iliamriwa kama mwafrika amemwona muasia au mzungu kuwa ni mzuri, basi aoe.

Waafrika kabla ya Mapinduzi hayo walitengwa na kukosa makazi bora tofauti na watu wa rangi zingine, hivyo zikafanyika jitihada za kuwawezesha wazawa kuwa na nyumba za kuishi. Matokeo ya mpango huo ni kuwapo maghorofa ya Michenzani, Unguja na mengine kisiwani Pemba.

Tangu kufanyika kwa Mapinduzi hayo miaka 61 iliyopita, kumeshuhudiwa mabadiliko makubwa ya kiuchumi, kisiasa na kijamii visiwani Zanzibar. Katika awamu zote za uongozi, kumekuwa na maendeleo makubwa katika masuala mbalimbali. Mabadiliko hayo yamesababisha wananchi kuwa na hali nzuri za kiuchumi. Kumekuwa na maendeleo ya miundombinu ya uchukuzi kama vile bandari, barabara na viwanja vya ndege ambayo imechochea kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi.

Sekta ya utalii imekuwa kichocheo kikubwa kwa maendeleo ya uchumi wa Zanzibar. Watu kutoka mataifa mbalimbali wamekuwa wakifika katika visiwa hivyo na kutembelea fukwe mwanana za Bahari ya Hindi zilizoko huko pamoja na vivutio mbalimbali na maeneo ya kale.


Hatua hiyo pia imevutia wawekezaji mbalimbali kujenga hoteli mbalimbali za kitalii kwenye visiwa vidogo na maeneo ya miji mikubwa. Ujenzi huo wa hoteli umechangia pato la taifa na kuboresha sekta ya utalii kwa ujumla.

Pia imeshuhudiwa uboreshaji wa huduma za afya na elimu Zanzibar mwaka hadi mwaka na sasa kuna mafanikio makubwa katika sekta hizo kulinganisha na kabla na baada ya Mapinduzi. Hospitali kubwa zimejengwa na huduma kuboreshwa huku katika elimu, shule nyingi kuanzia za awali mpaka sekondari zimejengwa na kuna wasomi wengi wa ngazi ya shahada hadi ya uzamivu kulinganisha na awali.

Aidha, kwa sasa kuna sera ya uchumi wa buluu ambao unashajihisha maendeleo endelevu ya kiuchumi kwa watu wa Zanzibar kupitia bahari kama vile uvuvi, kilimo cha mwani, utatifi na utafutaji wa gesi na mafuta. Kwa hakika Zanzibar ya sasa imenoga na Mapinduzi ambayo ni chanzo cha yote, yadumishwe na kuenziwa kwa vitendo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kundi hili liokolewe dhidi ya janga la afya ya akili



Na Sabato Kasika

**VIJANA** ni waathirika wakubwa wa tatizo la afya ya akili kutokana na sababu mbalimbali, zikiwamo msongo wa mawazo, matumizi ya dawa za kulevya na ugumu wa maisha unaosababisha baadhi yao kujiua.

Hayo ni kwa mujibu wa ripoti za afya ya akili za Wizara ya Afya katika kipindi cha mwaka 2022/23. Wagonjwa 138,625 wa afya ya akili walipatiwa matibabu ya ugonjwa huo katika vituo mbalimbali vya afya. Pia inaelezwa kuwa,watu milioni saba wana matatizo ya afya ya akili.

Kujiua kunatajwa kunashika nafasi kubwa kwa vifo vya vijana wa umri wa kati ya miaka 15 hadi 19, huku gharama kubwa za maisha na hali ngumu ya uchumi zikitajwa kuwa miongoni mwa sababu za ongezeko la tatizo la afya ya akili kwa kundi hilo ambalo ni taifa la kesho.

Kwa hali kama hiyo, kuna haja ya kufanyika kwa jitihada za makusudi ili kusaidia vijana kuepuka mazingira yote ambayo yanasababisha wakumbwe na tatizo la afya ya akili.

Vijana ndio taifa la kesho au nguvu kazi ya taifa, hivyo wakiwa katika mazingira hayo, ni wazi hawatakuwa na manufaa kwa taifa lao au wataendelea kupoteza maisha kutokana na sababu zinazochangia kuwapo kwa tatizo la afya ya akili.

Ni kweli vijana wanakabiliwa na vikwazo vingi kikiwamo cha ukosefu wa ajira, ambao inawezekana unawafanya wawe na hali ngumu ya maisha na hivyo kupata msongo wa mawazo hatimaye kujikuta katika tatizo la afya ya akili.

> **Vijana ndio taifa la kesho au nguvu kazi ya taifa, hivyo wakiwa katika mazingira hayo, ni wazi hawatakuwa na manufaa kwa taifa lao au wataendelea kupoteza maisha kutokana na sababu zinazochangia kuwapo kwa tatizo la afya ya akili.**

Ninajua kuna hatua mbalimbali zinazochukuliwa ikiwamo kufanya makongamano na midahalo ya kitaifa ili kuleta pamoja wataalamu na jamii kujadiliana masuala ya afya ya akili kwa jamii, watoto, vijana na makundi mengineyo.

Katika hatua hizo, inaelezwa kuwa yameanzishwa majukwaa huru matatu ya afya ya akili, kwa ajili ya kuendelea kutoa elimu kwenye jamii kuhusu afya ya akili na dawa za kulevya, lakini pia kuepusha sonona, kwa kuwa kati ya watu milioni saba, inaelezwa kuwa zaidi ya watu milioni 1.5 wanaishi na ugonjwa wa sonona.

Hatua hizo ni nzuri, lakini kama inawezekana, juhudi ziongezeke ili kunusuru vijana ambao kimsingi nguvu kazi ya taifa lolote, lakini sasa ndio wanaotajwa kukumbwa na tatizo hilo nchini.

Ni vyema vijana nao wakawa tayari kushiriki kwenye midahalo na makongamano, ili wapate mbinu za kuwawezesha kuepuka mazingira yanayowafanya wakawa na tatizo la afya ya akili.

Pamoja na hayo, vijana nao ni muhimu wawe makini na kuepuka kuingia katika makundi yasiyofaa kwani mwisho wake ni kujikuta wakiharibikiwa kwa kuwa na tatizo la afya ya akili.

Nje ya Tanzania, takwimu zilizowahi kutolewa na Shirika la Afya Duniani (WHO) na Shirika la Watoto Duniani (UNICEF) zinaeleza kila sekunde 40 mtu mmoja hufariki dunia kwa tatizo la afya ya akili.

WHO pia katika takwimu hizo, inaainisha kuwa vijana asilimia 20 ulimwenguni kote wana shida ya afya ya akili na katika nchi za kipato cha kati na chini karibu asilimia 15 wamefikiria kujiua.

MAKALA

FIKRA MBADALA

# Rais Samia, Mwinyi ponyeni makovu ya Mapinduzi kumaliza siasa za uhasama



Pascal Mayalla

LEO Januari 12, imedondokea siku ile ya Januari 12, 1964. Ilikuwa ni siku ya Jumapili kama leo. Katika siku hii, Watanzania wanaadhimisha miaka 61 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.

Wakati Wazanzibari wengi wanasherehekea kuyapongeza Mapinduzi hayo na wengine hadi kuyapa utukufu kwa kuyaita Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar, neno utukufu, ambalo kwa dini mbili kuu, Wakristo na Waislamu, anayestahili ni Mwenyenzi Mungu pekee. Kwa hiyo kuita kitu kingine chochote kitukufu ni kama kufuru!

Kuna Wazanzibari wengine, japo wachache, siku hii ni siku ya kumbukumbu mbaya, kwa kuwapoteza wapendwa wao kutokana na umwagaji damu wa Mapinduzi hayo na baada ya Mapinduzi. Hakuna ubishi kabisa kuwa Mapinduzi ya Zanzibar, yameleta heri, lakini ni ukweli mchungu pia yalisababisha maumivu makubwa kwa waliopinduliwa ambao wanaishi na makovu ya Mapinduzi.

Kule kwenye mtandao maarufu kuliko mitandao yote ya kijamii nchini Tanzania, Jamii Forums, shamrashamra za kuisubiria siku hii, zilianza siku nyingi kabla kushamirishwa na Fake News kuwa Sultan mpinduliwa anarejea Zanzibar kufanya ziara rasmi na atahudhuria maadhimisho ya leo.

Januari 9, 2025, Zanzibar itashuhudia tukio la kihistoria itakapompokea Sultan Jamshid bin Abdullah kurejea kwenye pwani zake. Hilo la Sultani kurejea mimi nikalidaka na kulitolea mapendekezo yangu 10 kwa SMZ.

Ndipo kaka yangu mmoja, kutoka Zanzibar, naomba kumtaja kwa jina moja tu Kaka Chalz, ni kaka yangu alinipokea RTD, akatufundisha kazi ya utangazaji, hivyo tunawaheshimu sana kaka zetu hawa, na hata tunapokosea, hawaachi kutupigia simu kuendelea kutuongoza mpaka leo mpaka kesho, Asante Kaka Chale!.

Basi Kaka Chalz akaniuliza una uhakika na chanzo chako cha habari kuwa hii ni habari ya kweli? Nikamjibu kwa vile imetangazwa na Jamiiforums, kwa jina maarufu JF, ni chombo cha kuaminika, ingekuwa fake, JF inatumia mfumo wa Jamii Check kubaini 'fake news' na kuzifuta, hivyo itakuwa kweli.

Ndipo nikaipitia ile habari kwa mara ya pili kusoma chanzo nikakuta ni jamaa yuko Oman! Nikamtafuta kaka yangu mwingine Zanzibar huyu ni Mzee Salim Said Salim, mwandishi wa siku nyingi, tunamwita jina la Mzee SSS, yeye ana nasaba kidogo na ukoo wa Sultan. Ukitaka kumtibua SSS, mwambie Mapinduzi Matukufu. Salim akawapandia kwa simu Oman, familia ya Sultan wakakanusha kuwa ni feki. Asante Mzee SSS.

Ndipo nikawasiliana na Mkuu Maxence Mello, chapisho langu likaondolewa ila chapisho la msingi halikuondolewa mpaka leo lipo. Nikamrudia Kaka Chalz, nikamshukuru kwa angalizo lake lakini nikamwambia baadhi ya yale mapendekezo yangu 10, mengine yako hai, yafanyiwe kazi. Baada ya hii 'fake news', jibu la familia ya Sultan alilotoa, ndilo likanijulisha bado kuna watu wana machungu na Mapinduzi yale. Wapoozwe.

Huu ni mwaka wa uchaguzi na hakuna ubishi siasa za Zanzibar licha ya uwapo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), bado zinaathiriwa na mzimu wa machozi, jasho na damu zilizomwagika na kufukiwa bila kufanyiwa hitima. Kuna watu wana makovu ya Mapinduzi yale.

Matokeo ya baadhi ya uchaguzi Zanzibar ni yale yale ya ule uchaguzi wa mwaka 1963. Mfano mzuri ni uchaguzi wa mwaka 2015, kuna msemo wa Kiingereza unaosema namba haziongopi!.

Matokeo ya iliyokuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) yamethibitisha pasina shaka kuwa uchaguzi wa Zanzibar wa 2015, kama usingefutwa, Maalim Seif Sharif Hamad wa Chama cha Wananchi (CUF) ndiye angelikuwa mshindi wa uchaguzi wa Rais wa Zanzibar kwa kutumia kigezo cha matokeo ya uchaguzi wa urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (JMT). Kule Zanzibar uchaguzi haukuwa na dosari.

Katika uchaguzi huo, mgombea wa UKAWA, Edward Ngoyai Lowassa, alimshinda mgombea wa CCM, Dk. John Pombe Magufuli. Katika matokeo hayo, Magufuli alipata kura 194,317 sawa na asilimia 46.5

na Lowassa kura 211,033 ambazo ni asilimia 50.50, kura halali zilikuwa 417,882.

Hii maana yake ni kwamba Zanzibar upinzani unaweza kushinda lakini kwa vile bado kuna machungu ya Mapinduzi, siku upinzani ukishinda Zanzibar, kutaibuka kulipiza kisasi!

Nashauri mambo yafuatayo;-

Kwanza, Zanzibar ianzishe tume ya ukweli na maridhiano ili watu waruhusiwe kutoa madukuduku yao. Pili, Desemba 10 iwe siku ya mapumziko ya uhuru wa Zanzibar. Si lazima iadhimishwe kwa shamrashamra bali naweza kubadili jina ikaitwa Sultan Day.

Tatu, neno Matukufu kwenye Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar lisiendelee kutumika bali yaitwe tu Mapinduzi ya Zanzibar na vibwagizo Mapinduzi Daima na Tutayalinda kwa gharama yoyote tuachane nayo ili kuponya wapinga Mapinduzi.

Nne, falsafa ya 4R za Rais Samia Suluhu Hassan itumike hadi Zanzibar. Mshindi wa kweli wa uchaguzi wa Zanzibar atangazwe.

Nawashauri Rais Samia na Rais Dk. Hussein Mwinyi kubalini kutibu makovu ya Mapinduzi ili kuzimaliza siasa za uhasama. Ikitokea upinzani umeshinda Zanzibar, hakuna haja kufunika kombe mwanaharamu apite. Iwe ni kupokezana kwa amani na upendo.

**Heri ya Mapinduzi.**
**Paskali**
**+255 754 270403**

KONA YA AFYA

# Ujue ugonjwa wa Homa ya Ini na athari zake



Na Dk. Mabula Budodi

HOMA ya ini ni ugonjwa unaoelezewa kuwa ni kuvimba kwa ini. Ini ni kiungo katika mwili wa binadamu kinachofanya kazi muhimu sana kama kuchuja, kupambana na hata kuondoa sumu mwilini.

Kuna vitu vingi vinavyoweza kusababisha homa ya ini lakini katika makala hii tutaongelea kuhusu homa ya ini inayosababishwa na virusi vya homa ya ini kama vinavyojulikana au kuitwa.

Katika nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, Tanzania ikiwamo, umekuwapo kwa miaka mingi lakini uelewa umekuwa mdogo na hafifu juu ya ugonjwa huu.

Hali hii inahusishwa na watu kutokuelewa ni nini hasa maana ya ugonjwa huu. Watu waliosoma pia wamekuwa na uelewa hafifu juu ya janga hili na wamefanana na wale ambao hawakupata bahati ya kupata mwanga wa kujua mambo ya kidunia- wasiokwenda shule.

Kwa sasa katika hospitali, vituo vya afya na makongamano ya kiserikali na yasiyo ya kiserikali, ikiwemo Siku ya Homa ya Ini Duniani, Julai 28 kila mwaka, watu wamekuwa wakiamshwa kuhusu uelewa wa ugonjwa huu. Watu wametafuta kujua hali zao mapema na hata kupata matibabu pale inapotakiwa.

**AINA ZA HOMA YA INI**

Kuna aina tano za Homa ya Ini ambazo zimepewa majina yao kutokana na herufi za alifabeti, yaani aina A,B,C,D,E.

Aina ya kwanza ya Homa ya Ini, yaani aina A, imeonekana kuambukizwa kwa njia ya chakula na mdomo, ikimaanisha kumpata mtu pale anapokula chakula kichafu kisicho safi na salama, chenye maambukizi ya virusi hivi vya homa ya ini. Pia kunywa maji au chakula kilicho na kinyesi ndani yake.

Aina hii ya virusi huambukizwa kwa urahisi na wepesi sana. Jambo zuri ni kwamba kuna chanjo yake ya kuzuia maambukizi ya virusi hivi.

Aina ya pili, yaani aina B, ni moja ya virusi vinavyoweza kusababisha madhara makubwa sana kama saratani ya ini au kushindwa kufanya kazi kwa ini lenyewe. Virusi hivi huambukizwa kwa majimaji ya mwili kama jasho na mate, manii wakati wa kujamiana, kwa damu kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto wakati wa kujifungua au ujauzito, kuchangia vitu vya ncha kali kwa kujichoma.

Pia aina hii ina chanjo ya kuzuia maambukizi yake lakini huweza kupewa pale tu unapoweza kupima kama tayari una maambukizi tayari au la. Chanjo yake huweza kutolewa siku ya kwanza baada ya kupima na kukutwa huna maambukizi hayo, baada ya mwezi moja, mitatu au sita baadaye.

Aina ya tatu ya virusi ya Homa ya Ini (aina C) hufanana na maambukizi ya aina B kwenye maambukizi na hata madhara ya baadae. Tofauti yake ni kwamba yenyewe haijapata chanjo yake mpaka sasa lakini ina matibabu yake. Matibabu yake huweza kuchukua wiki nane mpaka 12 kwa kutumia dawa za kutibu aina hii.

Aina ya nne ya Homa ya Ini (aina D), ni moja ya virusi visivyokuwa na chanjo mpaka sasa. Jambo zuri ni kwamba huwezi kuipata kama huna tayari maambukizi ya aina ya B, hivyo kama umepata chanjo ya kuzuia Homa ya Ini ya aina ya B, huwezi kupata aina hii pia. Aina hii pia huambukizwa kama ilivyo aina B na C.

Aina ya mwisho, yaani D, maambukizi yake huwa kama aina ya kwanza ya A, yaani kunywa maji machafu au yenye maambukizi ya virusi hivi au chakula kama nyama ambayo haijapikwa ikaiva vizuri. Aina hii ni hatari pale inapompata mjamzito kwa kuwa inaweza kusababisha madhara zaidi. Pia haina chanjo lakini huweza kuzuilika kwa kujikinga.

**DALILI ZA HOMA YA INI**

Dalili za Homa ya Ini zimekuwa zikifanana na dalili za magonjwa mengine hiyo imesababisha kuwa changamoto ya kujua kama kweli mtu ana ugonjwa huu tayari. Jambo muhimu zaidi kufanya ni kupima ugonjwa huu kwa njia ya damu kugundua kama una tatizo hili tayari na kuanza matibabu mara moja.

Dalili zake ni pamoja na kuhisi kuumwa,viungo na misuli kupasuka, mwili kuchoka na kuisha nguvu, kichefuchefu na kutapika, mwili kupata homa, macho kuwa ya njano, mwili kuwashwa, kupata mkojo mweusi kama chai au kupata choo kisicho na rangi.

KINGA NA MATIBABU

Matibabu ya Homa ya Ini kuweza kufanyika tu pale mtu anapogundulika kuwa na tatizo hilo. Ni ngumu kwa kuangalia na kujua kama mtu ana maambukizi tayari, hivyo inampasa mtu kupima ili kujua.

Kuzuia ni pamoja na kupata chanjo kwa aina zilizo na chanjo, kuzingatia usafi wa chakula na mazingira, kuepuka kufanya ngono zembe kwa kufanya mapenzi na mtu usiyemtambua afya yake, kuepuka kuwa na wapenzi wengi ambao huweza kuleta urahisi wa maambukizi na kuacha kuchangia vitu vya ncha kali.

Uelewa wa swala hili huweza kuzuia maambukizi mapya na kuzuia madhara ya baadae yanayoweza kukumba vizazi vyako vyote vijavyo. Fuata ushauri wa daktari wako na pima afya yako sasa.

**- Dk. Budodi ni daktari wa tiba ya binadamu na anapatikana jijini Dar es Salaam. Kwa ushauri unaweza kumpata kwa baruapepe mabulabudodi@gmail.com au simu namba 0710 980096**



Choo kilichojengwa mlimani juu ya miamba ambacho si salama hasa wakati wa mvua. **PICHA: VITUS AUDAX**

# Utapishaji vyoo waweka rehani maisha ya watu

INATOKA UK. 4

wamekuwa wakikabiliana nazo ni pamoja na magonjwa, harufu mbaya kwenye makazi ya watu pamoja na uchafuzi wa mazingira huku akitaka elimu itolewe juu ya athari za utiririshaji vinyesi katika mazingira.

**SERA YA MAZINGIRA**

Sera ya Taifa ya Mazingira ya 2021 Sura ya Kwanza kifungu cha Pili kifungu kidogo cha 6(1) kuhusu Usimamizi Duni wa Taka za Manispaa, inazitaja taka za maji kuwa tishio kwa mazingira na afya ya binadamu kutokana na kuwa vituo vingi vya mijini nchini havina vifaa vya usimamizi wa taka za maji.

Inafafanua kuwa kati ya Mamlaka 20 za huduma za maji mijini, 11 hutoa ufikiaji wa miunganisho ya mifereji ya majitaka na vifaa vya kutibu maji machafu. ikijumuisha takriban asilimia 13 ya wakazi wa mijini.

Polle anakiri kuwapo kwa baadhi ya wananchi ambao hawajaunganishwa katika mifumo na kuwa taratibu zinaendelea kufanywa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mwanza (MWAUWASA), kuhakikisha wanafikiwa na huduma kadiri bajeti inavyoruhusu.

Anasema wale ambao hawajaunganishwa wanatumia fursa ya mvua inaponyesha kufungulia vyoo vyao ili kuruhusu kinyesi kutiririshwa katika makazi ya watu pamoja na vyanzo vya maji likiwamo Ziwa Victoria.

Polle anasema wamekuwa wakitumia maofisa Afya wa ngazi za Halmashauri na Kata kutoa elimu kwa wananchi na kuhakikisha wanadhibiti utiririshaji maji taka hayo.

"Wananchi kwa kufanya hivyo wanakiuka kanuni na taratibu zetu na kawaida tunasema usafi ni tabia na uchafu ni aibu. Tunaendelea kuwapa elimu na kuwakumbusha kuwa kufanya hivyo wanaweza kupata adhabu kupitia sheria ndogo zilizowekwa na Halmashauri, anasema Polle.

**ATHARI KUBWA**

Kwa mujibu taarifa ya Mpango Kabambe wa Kitaifa wa Uhifadhi wa Mazingira kwa kipindi cha miaka 10 (2022-2032) kifungu namba 11 kifungu kidogo namba sita kuhusu Athari za Usimamizi Duni wa Taka, Tanzania inakadiriwa kuwa usafi duni unagharimu Sh. bilioni 301 kila mwaka sawa na Dola za Marekani milioni 206.

Hiyo ni sawa na asilimia moja ya pato la ndani la Taifa (GDP) la Tanzania na Dola za Marekani tano kwa mtu. Hasara za kiuchumi zinahusiana moja kwa moja na kupoteza muda kwa watu wanaotafuta mahali pa kujisaidia, vifo vya mapema, kupoteza uzalishaji wakati wa ugonjwa na fedha zinazotumika kwa huduma za afya.

Kadhalika, Shirika la Afya Duniani (WHO), linasema takriban asilimia tisa ya vifo vyote vya watoto chini ya miaka mitano na asilimia sita ya vifo katika idadi ya watu wazima, vinahusishwa na kuhara hali inayotokana na ukosefu wa miundombinu ya vyoo.

Ofisa Afya wa Jiji la Mwanza, Audiphace Sabbo, anasema katika kipindi cha robo ya Aprili hadi Juni, 2024 wagonjwa wa kuhara walikuwa 407 huku homa ya matumbo wakiwa wanane. Anasema Julai hadi Septemba, 2024 wagonjwa wa kuhara walikuwa 408 sawa na ongezeko la mtu mmoja huku homa za matumbo wakiwa 42 sawa na ongezeko la wagonjwa 34.

"Hii ni ishara ya kuwa watu wanakula uchafu maana Typhoid (homa za matumbo) ni uchafu, hivyo bado kuna tatizo na tunapopata hizi taarifa tunafuatilia kujua ni wapi wanatokea hivyo kwenda na kuchukua hatua," anasema Sabbo.

Aidha anataja maeneo korofi kwa uchafu na magonjwa ya mlipuko kuwa ni pamoja na Mabatini Kusini, Sinai, Majengo Mapya zote za Kata ya Mabatini, huku Kata ya Isamilo ikiwa na Mitaa ya Isamilo, Nyakabungo, Kaskazini 'A', Maendeleo na Msikitini, Kata ya Igogo ni Malulu, Kwimba, Jiwe la Maji na Bugando 'B'.

Kadhalika, Kata ya Luchelele iliyoko katika mwambao wa Ziwa Victoria, anataja Mitaa ya Silivin, Sweya na Kisoko huku Kata ya Mahina ni mitaa ya Mahina Kati na Igelegele. Kata ya Mkoloni ni Kasese, Nyamazobe na Utemini huku Kata ya Pamba ni Mitaa ya Mission, Bugarika 'C' na Mlimani.

"Hizi takwimu zinatokana na maeneo ambako wagonjwa wengi wa kipindupindu walitokea kwenye wimbi la mwaka jana, hivyo wagonjwa wengi walitokea kwenye hii mitaa na kuonekana ni michafu na kama Jiji tukajitahidi kuweka usimamizi ili isijirudie,"anasema.

Pia anasema kutokana na muingiliano mkubwa uliopo kwa Jiji la Mwanza suala la udhibiti na kutoa elimu ni endelevu kwani kila siku wanaingia watu wapya na wenye tabia tofauti.

**UCHAFUZI ZIWA VICTORIA**

Licha ya utiririshaji huo kutajwa zaidi kusababisha magonjwa, harufu mbaya pamoja na uchafuzi wa mazingira, hali hiyo inatajwa kuwa chanzo kikuu cha uchafuzi wa Ziwa Victoria, hivyo kuwapo hatari ya uhai wa viumbe hai waishio majini pamoja na watumiaji.

Utafiti uliofanywa katika Ziwa Victoria mkoani Mwanza na InfoNile kwa msaada wa JRS Biodiversity Foundation Machi, 2023 kupitia Mto Mirongo unaoingiza maji ziwani, ulibaini kuwapo kwa kiwango kikubwa cha kemikali ya E.Coli na Coliforms.

Utafiti huo uliitaja kemikali hiyo kusababishwa na wingi wa kinyesi katika mto huo unaoingiza maji ndani ya ziwa huku ikionesha kwamba maji yalikuwa yamechafuliwa na uwapo wa bakteria watokanao na kinyesi ambao wanaweza kusababisha magonjwa ya majini.

Ofisa Mahusiano kwa Umma wa Bodi ya Maji Bonde la Ziwa Victoria (LVBWB), Mhandisi Gerald Itimbula, anasema kwa sasa hakuna kiwanda chochote wala taasisi inayotiririsha majitaka ambayo hayajatibiwa katika Ziwa Victoria kutokana na takwa la kuweka mfumo wa kutibu maji hayo na kupimwa na maabara ya LVBWB kuhakikisha usalama wake ndani ya Ziwa.

"Kilichobaki kwa sasa ni wale wananchi wanaotiririsha majitaka hususani katika kipindi cha mvua. Ziko hatua za utekelezaji wa mradi mkubwa kupitia MWAUWASA utakaodhibiti kwa kiasi kikubwa kero hiyo," anasema.

**MAGONJWA SUGU**

Mkemia na Meneja wa Maabara ya Bodi ya Maji ya Bonde la Ziwa Victoria, Frank Baregu, wenye dhamana ya kujua hali ya maji, usalama wake na watumiaji katika eneo lote la bonde la Ziwa Victoria, anasema yako madhara ya muda mrefu na ya muda mfupi yatokonayo uchafuzi wa maji.

Anasema maji hayo yakitumiwa bila kutibiwa yanaweza kusababisha maradhi yakiwamo saratani, figo, misuli, tatizo la fahamu, ngozi kuungua akitolea mfano kwa tukio lililowakuta wakazi wa Mara pamoja na magonjwa ya kuhara.

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Uhusiano kwa Umma MWAUWASA, Vivian Temu, anakiri kuwapo kwa utiririshaji majitaka katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Mwanza. Anasema hali hiyo iko katika maeneo ambayo hayajafikiwa na miradi ya mfumo wa moja kwa moja wa majitaka.

"Baada ya kubaini hali ya uchafuzi, Mamlaka tulikuja na mfumo rahisi 'simplified sewerage system' kwa kuunganisha vyoo vyao kwenye mifumo yetu ya majitaka na kupeleka moja kwa moja kwenye mabwawa yetu ya kutibia majitaka katika eneo la Butuja," anasema Temu.

Pia anasema mfumo huo bado uko kwa maeneo machache yakiwamo Kilimahewa, Pasiansi, sehemu ya Mabatini, baadhi ya maeneo ya Igogo, Kabuholo, Ibungiro pamoja na Isamilo.

Anasema kutokana na gharama za kutengeneza mifumo hiyo kuwa kubwa sana mpaka sasa watu waliofikiwa bado siyo wengi kulinganisha na uhitaji ulivyo mkubwa.

"Wale ambao hawana mifumo hii wanatengeneza vyoo rahisi na vifupi kutokana na maeneo yao kuwa ya milimani na kuwa na mawe, hivyo wakati wa mvua wanafungulia yale majitaka yanaenda kwenye mito pamoja na Ziwa Victoria," anasema Temu.

ITAENDELEA

# MAISHA

JANUARI 12, 2025

Nipashe

Baba, Mama na Mwana *Jumapili*






# NENDA HIVI OFISINI



Ukurasa 13

# WATOTO

## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



| | | | |
|---|---|---|---|
| 2 | 4 | 3 | 1 |
| 1 | 3 | 4 | 2 |
| 3 | 1 | 2 | 4 |
| 4 | 2 | 1 | 3 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| B | ■ | J | U | N | G | U |
| W | ■ | ■ | ■ | O | ■ | B |
| A | ■ | T | I | N | ■ | W |
| W | A | O | ■ | D | O | A |
| A | ■ | L | A | O | ■ | B |
| N | ■ | E | ■ | ■ | ■ | W |
| I | K | O | M | E | ■ | A |


## FUMBO TOTO

Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:


DAI, MPO, MIA, FAA, SHIMO, DAMPO, EBOLA, MOSHI, ITWANGE, MTAFUNE

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | ■ | | | | | |
| | ■ | ■ | ■ | | ■ | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | | | ■ | | | |
| | ■ | | | | ■ | |
| | ■ | | ■ | ■ | ■ | |
| | | | | | ■ | |

## TOA TOFAUTI 5




## PAKA RANGI




## AMSHA AKILI

MDOGO WETU ANA UMRI WA MIAKA 6, BEGI LA SHULE LIMEWEKWA MBALI HAWEZI KULIFIKIA, HEBU TUMSAIDIE NJIA ILI AJIANDAE NA SHULE HAPO KESHO.



## CHEKA



Alichokifanya daktari

Msikie mtoto huyu akimuuliza maswali baba yake.

**Mtoto:** Baba unaweza kumwachia hilo gari lako dada wa kazi akaliendesha?

**Baba:** Siwezi kumwachia gari langu hili aliendeshe ni ghali sana.

**Mtoto:** Je, mnaweza kumwachia chumba chenu dada wa kazi kikiwa wazi na mkaenda kazini?

**Baba:** Haiwezekani kamwe, kuna vitu vya gharama na pia heshima haitakuwepo.

**Mtoto:** unaweza ukampa dada kadi ya ATM yako na namba ya siri ukakuchukulie pesa?

**Baba:** Mtoto una balaa wewe, unataka siku akiiba hii kadi akachukue pesa zote tuwe maskini, sithubutu.

**Mtoto:** aahaaaaaa, kumbe hauwezi kumkabidhi chochote chenye thamani dada wa kazi, sasa kwa nini mnanikabidhi mimi kwake nyie mnaenda kazini mpaka mnarudi, kumbe mimi sina thamani kwenu eeeeh

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Mume atajua thamani ya mke akiachwa

KARIBU tena msomaji wangu tuendeleze gurudumu la Maisha Ndivyo Yalivyo mwaka huu mpya. Bado naangazia nafasi ya wanaume kwenye ndoa zao.

Wiki mbili mfululizo nilimshauri mwanamume asimame kwenye nafasi yake ndoa ipone! Pia nikasema asikubali katu kulishwa na mwanamke!

Kwenye eneo hili, nikamtahadharisha mwanamume kwamba akikubali kulishwa na mwanamke atamdharau. Usipende kula chakula cha bure. Mwanamke hajaumbwa kutoa bali kupokea.

Siku ukila chakula cha mwanamke hujakitolea hela ya matumizi, kimbia. Unaweza kujikuta yuko mwanamume wa pembeni anayeilisha familia yako, jambo ambalo ni hatari sana.

Mungu alipomwumba mwanaume alimpa jukumu la kufanya kazi, ndipo baadaye akampa mke. Hivyo mwanamume ukitoka kafanye kazi na hakikisha hurudi nyumbani mikono mitupu. Familia inakutegemea urudi na chochote kitu (chakula).

Naam. Sasa tuendelee tuwasikie baadhi ya wanaume waliobahatika kusoma makala hizo nao wakatoa maoni yao kuhusu vyanzo vya mitikisiko kwenye ndoa nyingi.

Mtumishi mmoja wa Mungu akasema hivi: "Wanaume wamepewa heshima kubwa sana. Yesu ni mwanamume. Wanaume hawaitendei haki nafasi yao katika jamii. Wanaume tunakosea sana, tunaoa lakini hatujafundishwa. Wanaume wengine hata baba zetu hatuwajui! Wengi wanaanza maisha hawajijui.

"Kitu kingine hatujui kuwa wanawake wanataka nini. Mwanamke anapenda kuthaminiwa. Hata kama ni katika ujinga, wewe sema tu hapo safi. Msifie mkeo. Wanapenda vitu vya kijinga jinga...embe bichi.

"Kama hutaki ujinga usioe. Kwa asili mwanamke anahisi kaupungufu, ana nguvu ya kuongeza. Mwanamke mwonyeshe thamani yake. Akishagundua ni wa thamani kwako, atakuwa wako daima!

Akipatikana mtu anampa thamani yake, umeisha. Acha kuangalia makosa. Unamfanya aone unamshambulia. Na ukiachwa na mwanamke ndipo utajua thamani yake!"

Msomaji wangu, hebu sasa nikumegee baadhi ya mambo anayofurahia mwanamke toka kwa mwanaume. Nimesema hapo juu kwamba mwanamke anapenda kuthaminiwa.

Kuthamini maana yake ni kujali. Wanaume waliumbwa kujali. Ukiona mwanamke hajaliwi na mwanaume, tayari hapo ipo shida.

Pili, kupendwa. Lazima mwanamume aonyeshe kumpenda mkewe, kuvumiliana. Tatu, kutambuliwa jina na nafasi yake. Ana neema na karama gani. Hakuna kitu kibaya kama kutomthamini mtu/watu wengine.

Kitu kingine mwanamke anapenda toka kwa mwanamume ni kusemeshwa vizuri. Jifunze kumsemesha maneno mazuri. Usimkejeli, acha kumwambia mwenzio wewe ni ziro.

Mwanamke anapenda kukumbatiwa. Unaporudi toka kazini anapokupokea mkumbatie ishara ya upendo. Onesha uso uliochangamka.

Kingine wanawake wanapenda wanaume wasafi. Na jukumu lingine la mwanamke ni kuhakikisha mume wako ni msafi wakati wote, kimwili na kimavazi. Awe na mwonekano nadhifu siku zote.

Hata wanyama wengine wanatushinda kwa unadhifu. Mfano, Simba dume ni mzuri kuliko jike. Lina manyoya mengi kuvutia jike. Kadhalika jogoo na ndege tausi. Madume ni masafi.

Hata hivyo, simba dume hufa mapema kuliko jike kwa sababu ya msongo wa vurugu nyingi vichakani kusaka mawindo na ulinzi. Ni mtafutaji wa chakula.

Wanaume wanapenda kubembelezwa, hasa baada ya kazi ngumu wasemeshwe. Na ili watu waishi pamoja lazima mmoja aamue kushuka, vumilia ujinga (utani) maisha yaendelee". Mtumishi huyu anamalizia maelezo yake hivyo.

Msomaji mwingine aliyejitambulisha ni Mchungaji wilayani Bagamoyo naye anachangia maoni. Anasema kuwa, utii na upendo umekosekana katika ndoa nyingi.

Lakini pia anasema wanandoa wengi wanaoana kimaslahi. Mke anataka kujua kuna vitu gani kule ninakoenda kuolewa. Anapoingia na baadaye alivyovikuta vikatoweka, anatengeneza zengwe la kuondoka.

Mwanamke ana uwezo wa kumbadilisha mwanaume. Mwanaume ni jiwe linalopaswa kugeuzwa. Vaa sura ya Mungu uwe rohoni. Watu wengi wanaangalia vya dunia.

Ndoa nyingi ziko kwenye maslahi. Ili ndoa idumu lazima ujue ndoa ni kufurahishana na kuvumiliana kiasi, isizidi kero". Anamalizia mtumishi huyo.

Baadhi wasomaji wametuma ujumbe mfupi kupitia simu ya kiganjani unaosomeka, "Ubarikiwe sana kwa kuongea ukweli, endelea tupo nyuma yako" (0693730391). Mwingine anasema: "Asante kwa hekima zako na darasa zuri ulilolitoa. Mungu akubariki" (0623363916).

Mpenzi msomaji, bila shaka vipo vitu mbalimbali umejifunza kutokana na maoni ya watumishi hao wa Mungu na wasomaji wengine kuhusu ndoa. Tumshirikishe Mungu katika kila jambo kuponya ndoa zetu.

**Je, una maoni au kisa cha kimaisha/mahusiano ungependa tujadili pamoja? Tuma ujumbe mfupi 0715268581. Namba hii pia iko WhatsApp.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Vipande vya dinari na talanta vitazikwa hapa

KILA mtu ana safari yake ya kipekee maishani, yenye changamoto na mafanikio tofauti.

Ukilinganisha maisha yako na ya wengine, unaweza kujikuta ukishindwa kujivunia hatua zako au kushindwa kuthamini maendeleo yako.

Malengo na safari zetu ni tofauti. Kila mtu ana wakati wake wa kung'aa. Jifunze kuthamini hatua zako, hata kama zinaonekana ndogo.

Hakuna ubishi kwamba pesa na siasa zinaleta na kuondoa talanta za watu.Wawe wanaharakati, wanazuoni, wanasheria, wanamuziki na wanataaluma wengi unaowafahamu.

Vita Vya kisiasa humaanisha nini? ni hali ya kawaida ya migogoro ya uhasama iliyo wazi. Tamaa ya madaraka na umaarufu, kuwa na uwezo, mali na mafanikio yote ni sumu inayofanya kuwa mtumwa.

Ni lazima kuwa na macho kwa sababu hata pendekezo la udanganyifu nalo linakufanya kuwa mtumwa wa siasa za udanganyifu. Ni sumu ya tamaa ambayo uovu unataka kukita mizizi. Tamaa ya madaraka ikipungua, mtu anaweza kutumia nafasi yake kwa ajili ya kujenga taifa.

Je, kinachoendelea katika kampeni za Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ni propaganda au matusi? Huko CHADEMA bado makundi mawili yanawaunga mkono wagombea wakuu katika uchaguzi huo, wameendelea na kufanya kampeni zao nchi nzima.

Timu Lissu na timu Mbowe, zimeendelea kutafuta kura kila mahali. Mikoa kwa mikoa inajitangaza hadharani watamuunga nani mkono hata kabla ya kupiga kura. Hii si sawa kwa uhai wa demokrasia yetu.

Kinachoendelea sasa kwa makundi hayo mawili, viongozi na wanachama kutangaza hadharani, kunatishia uhai wa demokrasia. Kura zinaenda kupigwa za nini tena?

Kama mmeamua hivyo, kuna haja gani tena ya kupiga kura? Hata hivyo, mambo ambayo hayakutarajiwa ni kwamba baadhi ya watu katika timu hizo pamoja na baadhi ya wagombea au wagombea wote, wamekuwa wakitoa kauli juu ya maisha binafsi ya mgombea wa kambi nyingine.

Hata baadhi ya kauli hizo wachambuzi wa masuala ya siasa na demokrasia, wanapata shida kujua kama ni propaganda, kashfa au matusi.

Propaganda, ni neno lenye asili ya kilatini na limezaliwa kanisani, lakini likatekwa nyara na dunia ya siasa.

Propaganda ni sehemu ndogo ya mawasiliano ya umma (mass communication), yanayolenga kuathiri (influence) na kushawishi (persuade) hadhira au umma kwa kusudi maalumu, kutaka kupitisha mtazamo, ajenda au hoja ambayo haikubaliki na umma au hadhira.

Kimsingi kama huelewi, propaganda hufanya kazi ya kugeuza mtazao wa umma, juu ya jambo hilo ili lionekane kuwa ni zuri.

**Vita Vya kisiasa humaanisha nini? ni hali ya kawaida ya migogoro ya uhasama iliyo wazi. Tamaa ya madaraka na umaarufu, kuwa na uwezo, mali na mafanikio yote ni sumu inayofanya kuwa mtumwa.**

Propaganda hufanywa kwa kuchagua baadhi ya maneno, mambo na dhana ili kuubadilisha au kushawishi mtazamo fulani katika jamii. Mara nyingi propaganda hulenga zaidi katika kutaka kushawishi hisia badala ya fikra.

Kuna aina nyingi za propaganda, lakini ambazo zinajulikana sana ni propaganda za siasa na utawala. Kuna aina nyingi za propaganda, zikiwamo zile za kijeshi, za kiuchumi, za kijamii, za kidini na za kanisa.

Taasisi nyingi zina idara maalumu za propaganda, ambazo huweka bajeti kubwa sana kwa ajili hiyo. Idara hizo huwatumia watu maarufu katika jamii kwa njia ya kuwapa fedha pamoja na kudhamini kazi zao.

Si rahisi watu au umma kuweza kuwashtukia watu maarufu wanapokuja na wazo jipya, kuliko wazo lingeletwa na mamlaka moja kwa moja.

Kama hujui, lengo la propaganda ni kujenga hisia na taswira nzuri juu ya kitu, mtu, itikadi, chama au hata taifa.

Mtu anayetukana matusi, hasa katika kampeni kwa kiasi kikubwa anampunguzia kura nyingi mgombea wake, kwa kuwa wapiga kura huweza kufikiri kuwa mgombea ndiye aliyewatuma watu wake wakatukane mbele ya wapiga kura.

Katika kampeni zinazoendelea katika uchaguzi wa mwenyekiti wa taifa wa CHADEMA, wako baadhi ya wapigakura wamelalamika ya kuwa baadhi ya wapambe au wapambe, huwatisha wapigakura kuwa mgombea wao akishinda, atashughulika nao ambao hawakumpa kura.

Badala ya wao kunyenyekea kwa wapigakura, huwafokea na kuwatisha. Vitisho na matusi si sehemu ya propaganda.

*Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa simu namba 0715 545 490 au barua pepe: ghandsome79@gmail.com*

# HARUSI



Ilikuwa siku ya furaha wakati Thomas na Esther walipoamua kuaga ukapera na kufunga ndoa jijini Dar es Salaam hivi karibuni. PICHA: MC GaraB





MITINDO

Na Moshi Lusonzo



# NENDA HIVI OFISINI

MAVAZI ya ofisini kwa wanaume yana umuhimu katika mazingira ya kila siku ili kuepukana na kuvaa suti kila siku kama vazi maalum.

Kwa sasa kuna aina nyingi za mitindo ya nguo ambazo unapaswa kuvaa ukienda ofisini ikilinganishwa na miongo kadhaa iliyopita.

Hapo awali, mavazi ya ofisi ya wanaume yalikuwa suti pekee, lakini mambo yamebadilika kwani mtu anaweza kuvaa nguo yoyote ambayo inakubalika kutumika kazini.

Suti

Sasa kuna uwanja mpana wa kuchagua aina ya suti ambayo unaweza kuvaa, iwe suti ya kifungo kimoja, viwili hadi vitatu kwani chaguo ni lako tu.

Pia kuna suti za Kaunda suti iliyoshonwa na vitambaa vya aina mbalimbali vya kupendeza inatoa hamu ya kuvaa unapokwenda ofisini.

Suti za vipande vitatu na koti ni nzuri kama vazi rasmi la ofisini.

Mashati

Kuvaa mashati yaliyopangwa vyema na suruali inamfanya mtu kuwa na mwonekano maridadi na unaovutia zaidi.

Inashauriwa kuvaa shati yenye rangi tofauti na suruali nyeusi ili sehemu zote za mavazi ziwe wazi.


Katika kunogesha zaidi, weka tai nyembamba shingoni katika kunakshi vazi lako.



URELEMBO

## UREMBO
Na Mary Geofrey

# Tambua matatizo ya kucha



MIKONO viganja na vidole ni kati ya sehemu muhimu katika mwili wa mwanamke. Mikono hutumika kujiremba pamoja na majukumu mengine mengi.

Mikono isipotunzwa vizuri ni rahisi kuharibika, kupoteza mvuto wake wa asili na kuharibu afya ya kucha.

Hitaji la urembo wakati mwingine humsukuma msichana katika matumizi ya vipodozi vya kupaka kwenye kucha zake ili kukamilisha urembo wake.

Pamoja na kuwa kucha nzuri huongeza urembo, mvuto na furaha ya mwanamke lakini pia ni vizuri kukumbuka kuwa afya ni muhimu kuliko urembo na uzuri.

Kufifia kucha

Endapo rangi ya kucha zako ikiwa kama imefifia hivi basi kuna uwezekano mkubwa wa kuwa na tatizo la ukosefu wa damu, vile vile inaweza kuwa ni tatizo la kisukari au magonjwa ya Ini.

Kucha za njano

Endapo kucha zako zikiwa na muonekano wa rangi ya njano basi utakuwa una tatizo la fangasi kwani ndiyo chanzo kikuu cha kucha kuwa za njano. Lakini pia unaweza kuwa na tatizo la Tezi.

Tafiti zinaonesha kuwa tezi hili la shingoni husababisha kucha kutokuwa na afya zuri kwasababu thyroid homoni zinasababisha kucha kutengana na ukuta (mzizi wake) hivyo kupelekea kucha kushindwa kukua vizuri matokeo yake muonekano wa kucha unakuwa ni kama kwenye picha.

Kucha za bluu

Ubluu katika kucha nalo ni tatizo, hii inawezekana ukawa na tatizo katika mfumo wa hewa.

Kuwa na kucha za rangi ya bluu ni matokeo ya ukosefu wa oxygen katika kucha zako.

Hii inasababishwa na kuwa na mzunguko mdogo wa damu hasa katika maeneo ya baridi sana.

Kuwa na mzunguko mdogo wa damu kunasababisha damu isifike katika maeneo yote ya mwili kwa kiasi kinachohitajika.



## MAPISHI
Na Mary Geofrey

# Samaki wa Salmon

KUTOKANA na majukumu mengi ya kila siku, foleni za barabarani, unafika nyumbani umechoka na hivyo kushindwa kuwa na muda wa kutosha kupika chakula unachokipenda.

Katika safu yetu ya mapishi tutakuelekeza njia rahisi na salama ya kupika chakula rahisi samaki aina ya Salmon Fillet.

Mlo huu ni rahisi kuuandaa na hata haikuchukui zaidi ya dakika 20 chakula kinakuwa tayari mezani.

**Mahitaji**

Salmon fillet 2, viazi mviringo kiasi, Lettice kiasi, nyanya iliyosagwa, limao 1, kitunguu swaumu, chumvi na mafuta ya mzaituni.

**Namna ya kupika**

Mmarinate samaki na chumvi, swaumu na nusu ya limao kisha muweke pembeni, baada ya hapo washa oven kisha tia potato wedge zikishakaribia kuiva anza kumpika samaki, tia mafuta kidogo sana kama kijiko kimoja cha chai hivi katika frampeni isiyoshika chini.

Mafuta yakishapata moto kiasi muweke samaki wako (upande wenye ngozi chini kwanza) mpike mpaka uone rangi ya kahawia kwa chini kisha mgeuze upande wa pili, huku samaki wako akiwa anaendelea kuiva.

Tayarisha salad yako kwa kusafisha lettice na nyanya kisha zichanganye pamoja kisha tengeneza saladi pembeni, kamua limao kisha weka mafuta ya mzaituni na chumvi kidogo.

Baada ya hapo samaki na potato wedge vitakuwa vimeiva, andaa mlo wako na utakuwa tayari kwa kuliwa.



MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Kujenga nyumba ni kuweekeza

UJENZI wa nyumba ni uwekezaji kama ulivyo uwekezaji mwingine wowote. Kwa maana hiyo, mtu anapojenga nyumba, iwe ya kuishi au ya kupangisha, anakuwa anawekeza fedha zake katika kitu cha thamani.

Kupitia nyumba ya kuishi, mtu anakuwa na amani kwamba hana tatizo la makazi. Pia anapokuwa na nyumba ya biashara (kupangisha) anajiongezea kipato kutokana na kodi ya pango la nyumba hiyo.

Wako watu ambao wamekuwa wakidai kuwa nyumba ya kuishi ni mzigo kwa sababu haimwingizii mtu chochote. Ukweli ni kwamba madai hayo hayana mashiko kwa sababu mtu anapokuwa na nyumba hiyo, anaweza kupata mkopo katika taasisi ya fedha na hatimaye kufanya biashara ambayo itamwongezea ukwasi.

Pamoja na ukweli huo, ni vigumu sana kufanikisha kuwa na nyumba ya ndoto yako endapo hujaweka mipango mizuri ya kuwekeza pesa kwa ajili ya kutimiza azma hiyo.

Mtaalamu wa ujenzi, Khamis Ally, anasema viko vitu ambavyo mtu ambaye amekusudia kuwekeza kwenye ujenzi wa nyumba anapaswa kuvifahamu.

Moja ya vitu hivyo, anasema ni kuweka mipango madhubuti juu ya ujenzi wa nyumba katika mtazamo wa sasa na wa baadaye.

"Unapopanga kujenga nyumba yako ni muhimu kuiona baadaye na mabadiliko yake. Ni vyema ujue jengo lako litakavyokuwa kabla ya kuanza ujenzi. Ufahamu uzuri wake, ukubwa, kimo, rangi.

"Pia ujue ni wapi utakwenda kununua vifaa vya ujenzi kama vile saruji, mbao na nondo. Umfahamu fundi atakayekujengea, ukanda unaojenga ni





wa aina gani kijiografia na ufahamu kama eneo lako halina mgogoro wowote iwe ni kwa upande wa serikali au majirani," anasema.

Jambo lingine ambalo mtaalamu huyu anashauri ni kujenga nyumba inayokidhi mahitaji yako.

Ni muhimu kufahamu ni nyumba ya aina gani unayotaka kujenga kwa kutazama mahitaji yako katika uhalisia wa sasa na wa baadae na kumshirikisha mtaalamu aliyebobea katika usanifu wa nyumba za kuishi.

"Kujenga kwa kuzidi mahitaji yako, inaweza kuleta hasara ya kushindwa kumaliza ujenzi. Unaweza ukajiuliza maswali kadhaa. Je, kuishi kwenye hiyo nyumba ni faida zaidi kuliko kupanga? Ni muhimu kuhakikisha kwamba unajenga kwa faida na si hasara.

"Baadhi wamejikuta wamejenga nyumba ambayo inadumu kwa muda mfupi, wapo waliofikiri kutumia vifaa duni vyenye gharama ndogo ndio namna ya kupunguza gharama na badala yake walijikuta wakihitajika kuvibadili baada ya muda mfupi na kwa gharama kubwa zaidi. Wapo pia waliochakachua kwa kujua kwamba ndio njia nzuri ya kupunguza gharama, na kujikuta katika hatari za nyufa, kubomoka na kutokudumu kwa muda unaofaa," anasema.

" Hakikisha unakuwa na mtazamo wa kiuchumi wa kujenga kilicho bora, imara, kinachodumu na kwa gharama nafuu," anasisitiza.

Ally anasema kwamba kabla ya kuanza ujenzi wa nyumba yako, ni vizuri pia ukadodosa na kupata taarifa sahihi zinazohusiana na ujenzi ikiwamo gharama ambazo hutumika kulipa mafundi, vifaa vinavyopaswa kununuliwa ili kukusaidia kufanya uamuzi bila hofu na usionekane hujui chochote mbele ya mafundi wako na wakatumia mwanya huo kukudanganya baadhi ya vitu.

Pia anashauri kuhakikisha unasimamia ipasavyo ujenzi wa nyumba yako unapoanza hadi unapomalizika ili kuhakikisha kila kitu kinakwenda kama kilivyopangwa badala ya kuwaachia huru mafundi.

# Fukuza nyoka kwa mimea hii

Na Restuta James

UNASUMBULIWA na nyoka au wadudu wakali? Je, nyumba yako iko kwenye mazingira ambayo nyoka anaweza kuingia? Usiogope. Ipo mimea ambayo inaweza kuwafukuzia mbali na kukuhakikishia usalama.

Licha ya kwamba baadhi ya mimea inastawi vizuri zaidi kwenye maeneo ya baridi, lakini mchaichai, vitunguu (swaumu na maji), ulimi wa mama mkwe na marigold, inaweza kustawahi katika mazingira yote.

Mimea hii inatajwa kuwa na uwezo wa kufukuza nyoka kutokana na harufu kali inayomkosesha raha nyoka, hivyo kumfanya asisogee kwenye eneo au bustani yako.

MARIGOLD

Wataalamu wanaeleza kuwa harufu yake na mizizi ya marigold huwafukuza nyoka.

Mkulima katika kijiji cha Onana, Kata ya Kibosho Magharibi, mkoani Kilimanjaro, Peter Massawe, anasema aina hiyo ya ua huwafukuza pia wadudu waharibifu wa mazao ya mbogamboga na nyoka.



"Shambani kwangu nimeyapanda sehemu tofauti tofauti ili kulinda mazao. Ni mazuri ukipanda nyumbani kwa sababu unafukuza nyoka," anasema.

Anataja mmea mwingine ambao pia umetajwa na wataalamu wa kilimo kuwa ni mchaichai.

Wataalamu wanaeleza kuwa mchaichai unapokatwa, hutoa harufu kali ambayo huwasumbua nyoka.

"Hata kama nyoka ameshaingia kwenye eneo lako, ukiwa umevuna mchaichai ile harufu inamsumbua kwa hiyo ataondoka tu," anasema.


Katika orodha hiyo, lipo ua la ulimi wa mama mkwe (snake plant), ambalo linaogopwa na mnyama huyo. Ni ua linalopaswa kupandwa katika kila nyumba kutokana na uwezo wake wa kuzalisha hewa safi ya oksijeni na kufukuza wadudu wasumbufu.

Mmea mwingine unaotajwa na wataalamu ni vitunguu maji na swaumu, ambavyo vinawafukuza nyoka kwa harufu yake.

"Nyoka ni wageni wasiokubalika katika mazingira ya nyumbani, ikiwa unajiuliza jinsi ya kuwazuia, mimea ambayo ni dawa asilia isiyo na kemikali, ni suluhisho salama zaidi," anasema Massawe.

Anasema mimea hiyo ni rafiki wa mazingira, huleta harufu nzuri nyumbani na chakula kwa ajili ya afya.

# KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2025
SMS - 0713 447766
"VITA UENYEKITI" MAMBO YA NGOSWE HA HA HAAAA
JUKWAANI
HIVI BABU ULIPOKUWA KIJANA ULIWAHI KUWA HENDISAMU?
HENDISAMU 'JESHINI!?'
GONGO SIO POMBE YA KUIENDEKEZA MAINI YANAKUFA
KWANI NIMEKUOMBA SANDA?
MWANAMKE RAHAAAA! KUDANGA MPAKA KUTOBOA MWAKA SIO MCHEZO 'PIIIJAAAA KEEERERЕЕЕЕ KWA MADANGA'AKEEEEE!
ULIKEMEA SANA UNYWAJI WA GONGO!
BAADA YA KUSTAAFU NATAKA NYIE MNIKEMEE
NASEMA HIVIII MKEO ASIKUSUMBUE PIGA KISHA MPE TALAKA!
KAMA KAFUMANIA AANZE NA MGONI WAKE... LAKINI KAUNGUZA MBOGA NO KES!
WE' HASARA KABISA HUFAI HATA KIDOGO!
ZOTE KESI TU!
LABDA HUYO MWANAWE KAFUMANIA? ACHEKELEE!
KWANI NYIE HAKIMU?
BICHWA LAKO BAYA!
SIKU MOJA SOGELEA KIOO!
ACHA KUJIENDE-KEZA...MAUMIVU YA SINDANO TU?
SINDANO MOJA NIME-PATA SABAU YA KUKUDEKEA WAIFU...
*KINYUNYIZO CHA LEO...
KUWA SHUJAA KAMA MLEVI KWENYE HATARI...

HABARI KIMATAIFA

## Moto wazidi kuleta hofu Marekani

**CALIFONIA,** MAREKANI

MAMLAKA ya jimbo la Califonia nchini Marekani imetangaza amri ya kutotembea nje katika maeneo ya Los Angeles kwa ajili ya kulinda mali katika makazi na majengo ambayo watu wamehamishwa kutokana na moto mkali unaoendelea kuwaka.

Gavana wa California, Gavin Newsom, aliomba kufanyika uchunguzi huru katika Idara ya maji na umeme ya mji wa Los Angeles.

Uchunguzi unahusu kuwepo kwa uhaba wa maji kwenye idara ya zimamoto huku wazimamoto wakikabiliana na moto mkali unaoteketeza nyumba na miundombinu ya mji katika mji huo wa kifahari wa Marekani.

Gavana Newsom alisema ripoti za upungufu wa maji na ukosefu wa usambazaji wa maji kwenye hifadhi muhimu zinasumbua.

Alisema uhaba wa usambazaji wa maji kwa kutumia mabomba ya maji huenda ukadhoofisha juhudi za kulinda baadhi ya nyumba na njia za uokoaji.

Tayari watu 10 wamekufa kufikia jana kutokana na moto huo.

**DW**

## Uturuki yataka Ufaransa iwachukue wafungwa wake

**ANKARA,** UTURUKI

UTURUKI imeomba Ufaransa kuwarejesha nyumbani wanamgambo wa jihadi wa nchi hiyo wanaozuiliwa na wanajeshi wa Kikurdi nchini Syria.

Katika mkutano na waandishi wa habari Waziri wa Mambo ya Nje wa Uturuki, Hakan Fidan, alisema wanachozingatia kwa sasa ni usalama wa raia hao wa Ufaransa.

Uturuki inawashutumu wanamgambo hao kuhusishwa na kundi la PKK, ambalo Uturuki inaliona kuwa la kigaidi.

Kwa miaka mingi, kumekuwepo kwa uungwaji mkono wa nchi za Magharibi na Marekani kwa vikosi vya Wakurdi nchini Syria.

Hata hivyo, Waziri huyo wa Uturuki aliishutumu Ufaransa kwa kuweka tu masilahi yake mbele.

"Wana sera ya kwamba hawaleti wafungwa kutoka kundi la kijihadi la Islamic State katika nchi yao. Lakini hawajali usalama wetu," alisema.

Alisema vikosi vya Kikurdi, YPG, vilipigana dhidi ya kundi la Islamic State na kwamba wanalinda kambi za magereza ya kijihadi kama kisingizio cha kuachwa kuendelea kuwepo Syria.

"Ikiwa Ufaransa ina lolote la kufanya, ni lazima kuwachukua raia wake na kuwaleta kwenye magereza yake na kuwahukumu katika mahakama zake. Sio juu ya kuwakabidhi kwa mamlaka ya magereza ya YPG au kundi lingine la kigaidi, na kisha kuja na kusema kwamba wanaunga mkono kundi hilo," aliongeza.

**RFI**

# Watoto milioni 3.2 hatarini kupata utapiamlo Sudan

**KHARTOUM,** SUDAN

UMOJA wa Mataifa unaendelea kuonya kuhusu hali mbaya ya ukosefu wa chakula inayoikumba Sudan.

Kulingana na Shirika la Kuhudumia Watoto Duniani, watu milioni 12 wamekimbia makazi yao kutokana na mapigano yanayoendelea.

Shirika hilo lilisema mwaka huu zaidi ya watoto milioni tatu walio chini ya umri wa miaka mitano wako katika hatari ya kukabiliwa na utapiamlo mkali nchini kutokana na kukosa chakula.

Baa la njaa tayari limeikumba nchi hiyo ambayo vita inatarajiwa kuenea nchi nzima.

Vita hivyo vilivyoanza Aprili 15, 2023 kati ya jeshi la Sudan na wanamgambo wa Vikosi vya Msaada wa Haraka (RSF), vinaathiri moja kwa moja raia.

Umoja wa Mataifa unaomba dola bilioni 4.2 kwa ajili kusaidia raia wa Sudani.

Watoto 772,000 walio chini ya umri wa miaka mitano wako katika hatari ya kupata utapiamlo mkali katika kipindi cha mwaka mmoja unaokuja.

**Aina hiyo ya utapiamlo inahatarisha watoto 3,200,000 wa rika moja nchini humo, kulingana na UNICEF. Upatikanaji duni wa huduma za matibabu na maji safi, mazingira machafu, njia zisizofaa...**

Aina hiyo ya utapiamlo inahatarisha watoto 3,200,000 wa rika moja nchini humo, kulingana na UNICEF.

Upatikanaji duni wa huduma za matibabu na maji safi, mazingira machafu, njia zisizofaa za ulishaji wanyama na kuenea kwa ukosefu wa chakula ni sababu kuu za kuenea kwa utapiamlo mkali.

Njaa hiyo iliyoanza miezi minne iliyopita tayari imekumba mikoa mitano ya Sudani, kulingana na mashirika ya Umoja wa Mataifa, lakini inaweza kuenea katika mikoa 17 ifikapo mwezi Aprili. "Sudan ndiyo nchi pekee duniani ambako njaa imethibitishwa. "Njaa na baa la njaa vinaenea kwa sababu ya maamuzi yanayofanywa kila siku kuendeleza vita hivi, bila kujali gharama kwa raia," amesema Edem Wosornu, mkurugenzi wa operesheni wa Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Masuala ya Kibinadamu.

Matatizo katika kupeleka misaada ya kibinadamu nchini Sudani yanaweza kusababisha utapiamlo kuwa mbaya zaidi, kwani vita nchini Sudani tayari vimewakosesha makazi watu milioni 12, na kuifanya kuwa janga kubwa zaidi la wakimbizi duniani, kulingana na Umoja wa Mataifa.

**RFI**



Mwanajeshi wa Russia akilenga shabaha dhidi ya vikosi vya Ukraine kwenye mapigano katika mkoa wa magharibi wa Kursk juzi. **PICHA: AP**

# Maduro aanza muhula mwingine urais Venezuela

**CARACAS,** VENEZUELA

RAIS wa Venezuela, Nicholas Maduro, ameapishwa kuendelea na nafasi hiyo kwa muhula wa tatu wa miaka sita.

Nicholas Maduro amekuwa madarakani tangu 2013. Kuapishwa kwake kunakuja baada ya tume ya uchaguzi kumtangaza mshindi katika uchaguzi uliofanyika mwezi Julai, mwaka jana.

Ushindi huo uliidhinishwa na mahakama ya juu nchini humo, licha kambi ya upinzani na nchi za magharibi kukosoa uchaguzi huo.

Hata hivyo, matokeo kamili ya kura hiyo hayajachapishwa rasmi.

Kiongozi wa upinzani nchini Venezuela anasisitiza takwimu za kura zinaonesha aliyekuwa mgombea wao, Edmundo Gonzalez, ambaye pia anaungwa mkono na serikali za Magharibi, ikiwemo Marekani, zinamtambua kama rais mteule kwa kuwa alishinda.

Gonzalez alikimbilia Uhispania, lakini ameahidi kurejea Venezuela kuchukua madaraka.

Wakati wa zoezi la kuapishwa kwa Maduro, serikali ya Venezuela ilifunga mipaka na anga yake na Colombia kwa muda wa saa 72. Hayo yamesemwa na wizara ya mambo ya nje ya Colombia.

Waziri Mkuu wa Italia, Giorgia Meloni alipinga kile alichokitaja kuwa kurejea kusikokubalika kwa ukandamizaji nchini Venezuela.

Kwenye taarifa yake, Meloni alisema wanakusudia kuhakikisha kuna ukabidhianaji madaraka kwa amani na kidemokrasia na kwamba matumaini ya uhuru na demokrasia ya Wavenezuela ni sharti yatimizwe.

**DW**

# Ujenzi barabara kiwango cha lami kuipaisha Moro

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKARI kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) imetenga Sh. bilioni 320.558 kwa ajili ya ujenzi wa barabara kiwango cha lami zenye urefu wa kilometa 189.6 katika Mkoa wa Morogoro ili kukuza uchumi kupitia sekta ya kilimo.

Meneja wa Wakala TANROADS Mkoa wa Morogoro, Mhandisi Alinanuswe Kyamba, alisema hayo juzi kwenye kikao cha 42 cha Bodi ya Barabara ya Mkoa wa Morogoro kilichofanyika mjini hapa.

Mhandisi Kyamba alizitaja barabara hizo na urefu wake katika mabano ni Ifakara- Mbingu (km 62.5), Mbingu- Chita (km 37.5), Bigwa - Mvuha ( km 78) na Ubena Zomozi - Ngerengere (Kizuka Amy Camp) kilometa 11.6.

Alisema serikali imetenga Sh. bilioni 37.841 kupitia ufadhili wa Benki ya Dunia ili kujenga madaraja maeneo ya Chakwale, Nguyami katika wilaya ya Gairo.

Alitaja madaraja mengine kuwa ni Mjonga, Bwage na Doma yaliyoko katika wilaya ya Mvomero, Ngerengere na Kihonda katika wilaya ya Morogoro.

Mbali na fedha hizo, Mhandisi Kyamba alisema Sh. bilioni 16.153 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa madaraja ya Namhanga na Fuluwa, hivyo kufanya jumla ya fedha kuwa Sh. bilioni 53.994.

Mhandisi Kyamba alisema katika kurejesha mawasiliano katika barabara na madaraja yalioathiriwa na mvua ya EL-nino na kimbunga cha Hidaya, serikali ilitoa kiasi cha Sh. bilioni 4.716.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alisema mkoa huo unaweza kupiga hatua zaidi kiuchumi iwapo miundombinu ya barabara itakuwa na ubora wa kupitia msimu wote wa mwaka.

Malima aliitaka TANROADS na Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) kuimarisha miundombinu ya barabara katika maeneo ambayo ni korofi.

Aidha, Mkuu wa Mkoa aliitaka TARURA kushirikiana na mabaraza ya madiwani katika utekelezaji wa bajeti ili kuwa na uelewa wa pamoja.

# Othman ataka misikiti kukuza tabia njema

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wsa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema misikiti inayojengwa katika maeneo mbalimbali nchini inapaswa kuwa mahali sahihi pa ibada, kulea imani na kukuza tabia njema kwa waumini wa Kiislamu.

Othman aliyasema hayo juzi Kijuki Pandani, Kaskazini Pemba, alipowasalimia waumini wa Dini ya Kiislam baada ya kufungua msikiti mpya wa Ijumaa wa Kijiji hicho uliopewa jina la Masjid Nuur Muhammad, alipojumuika nao katika ibada ya swala ya Ijumaa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kitengo cha Habari Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, Othman alisema vyema waumini wakafahamu kwamba wanapaswa kutambua kuwa misikiti si tu kwamba ni mahala pa kufanyia ibada pekee, bali pia inapaswa itumike kuwa sehemu muhimu ya malezi ya nafsi na kitalu cha kukuzia tabia njema ambazo zinapaswa kusomeshwa ndani ya msikitini kwa kufundishwa vijana.

Alisema katika maeneo mbalimbali ya Zanzibar, kumekuwepo jamii ya vijana kuharibika kitabia na watu kujali kupata tu hata ikiwa ni haramu, jambo linaloatiri mustakabali na jamii kwa kusindwa kujenga imani ya kweli kwa watoto na vijana.

**Makamu wa Kwanza wa Rais alisema mambo wanayofanya watoto na vijana kinyume cha maadili ya jamii na usilamu ni makubwa kutokana na kuharibikiwa kimalezi. Alisema jamii inapaswa kutimiza wajibu wake ...**

Makamu wa Kwanza wa Rais alisema mambo wanayofanya watoto na vijana kinyume cha maadili ya jamii na usilamu ni makubwa kutokana na kuharibikiwa kimalezi. Alisema jamii inapaswa kutimiza wajibu wake wa kuwalea vyema watoto ili kujenga kizazi chema na kuimarisha Uislamu.

Aidha, aliwahimiza waumini wa dini ya Kiislamu kutoa swadaka mbalimbali kwa walichoruzukiwa ili kutegemea malipo mema kwa Mola wao aliyewaruzuku mali za aina mbalimbali na kwamba ni vyema pia kushindana katika kutenda mambo mema ili kuipeleka mbali dini yao.

Akitoa salamu za Ofisi ya Mufti, Sheikh Said Ahmed, aliwasihi waumini wa dini ya Kiislamu nchini kutambua kwamba kuwapo kwa neema kujengwa kwa misikiti mipya mizuri, kusilete mifarakano miongoni mwa waumini na badala yake izidishe umoja miongoni mwa waumini na yakitokea hayo, furaha ya misikiti mipya inageuka kuwa huzuni.

Sheikh Said aliwataka Waislamu kutambua kwamba Waislamu wote ni ndugu na ndio msingi wa ibada na dini yao kwa mujibu wa mwongozo wa Mtume Muhammad SAW na kwamba wanapaswa kusaidiana kwa hali na mali ili kufanyiana wepesi kwenye shida na kukingiana mabaya.

Akisoma risala mbele ya mgeni rasmi, Ustadhi Hafidh Said Omar aliwashukuru wafadhili mbalimbali kwa kufanikisha ujenzi wa msikiti huo kwa kipindi cha muda usiozidi mwaka mmoja na kuomba wasaidiwe kifusi cha kuondoa tope katika kipande cha njia ya kuingia kwenye msikiti huo.

## BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Jamaa aliyetongoza demu, kesho akakuta msiba wake



**Na Adam Fungamwango**

**Akavutiwa naye na akaamua kutoa la moyoni. Msichana naye wala hakuwa na tatizo. Akamkubalia jamaa. Kama vile haitoshi, akamuonesha anapoishi. Haikuwa mbali sana na hapo walipokutania. Mitaa ya Ilala yote ina majina, na namba za nyumba, akamtajia.**

DUNIA ina mambo mengi. Ina mikasa mingi ambayo mingine unaweza kudhani kama ni hadithi tu za Alfu lela Ulela, au za kusadikika. Lakini mengi yanayotokea duniani, yapo ya kupendeza, kuchekesha, kuhuzunisha na kusikitisha. Likikupata jambo baya, unaweza ukadhani kuwa una mkosi kuliko watu wote duniani.

Unaweza kujichukia na kutaka hata kujidhuru. Ukija kuhadithiwa kisa kilichompata mwingine unajikuta kuna afadhali chako. Kidogo inaweza kukufariji kuona kumbe linalokupata wewe linaweza kumpata mwingine duniani.

Leo tutaangalia mkasa wa jamaa mmoja ambao umesimuliwa katika wimbo wa Tanzania Stars, uitwao 'Mawazo.'

Ulirekodiwa mwanzoni mwa miaka ya 1980, na kuwa moja ya nyimbo zilizopendwa na mashabiki wengi.

Bendi hiyo kwa wakati huo ilikuwa bado haijawa maarufu sana masikioni mwa mashabiki, lakini wimbo huo uliondokea kuwa maarufu zaidi kuliko bendi yenyewe.

Ukaifanya bendi hiyo kuanza kujulikana. Ilikuwa hivi. Jamaa mmoja katika pitapita zake mitaa ya Ilala, Dar es Salaam, akakutana na msichana.

Akavutiwa naye na akaamua kutoa la moyoni. Msichana naye wala hakuwa na tatizo. Akamkubalia jamaa.

Kama vile haitoshi, akamuonesha anapoishi. Haikuwa mbali sana na hapo walipokutania. Mitaa ya Ilala yote ina majina, na namba za nyumba, akamtajia.

Kesho yake kama walivyopanga aende nyumbani kwake akamtembelee wapige stori na kuyaweka mambo yao sawa, ilifika.

Akaenda mpaka Ilala. Akafika mpaka kwenye mtaa na nyumba aliyooneshwa.

Kilichomshangaza kidogo, akakuta watu wengi, na kuna turubai. Akili ikamwambia kuwa kuna kitu, ama sherehe za kijamii, au msiba. Na kweli kimoja wapo kilikuwepo. Ulikuwa ni msiba.

Hakuwa na wasiwasi sana kwani alijua nyumbani kwa mpenzi wake kuna msiba, hivyo asingeweza kuonana naye mpaka siku nyingine. Wakati anajiandaa kuondoka, akapishana na mtu ambaye alionekana kutoka mle ndani.

Akamsalimia na kuuliza kuna nini? Akamwaambia kuna msiba. Akaamua tu kuuliza wa nani. Jina alilotajiwa lilikuwa ni la yule mpenzi wake.

Akashtuka. Akauliza tena. Akajibiwa kama mwanzo. Akaanza kuelezea wajihi wa msichana ambaye amefariki kama ndiyo huyo au mwingine.

Yeye aliutaja. Akaambiwa ndiyo huyo huyo. Hakuridhika.

Mwenyeji naye akamtajia wajihi huo huo na kuongezea vitu vingine kama sauti na mengine ambayo jamaa sasa aliamini kuwa aliyefariki si mwingine ila ni mpenzi wake.

Nguvu zilimuishia. Alikwenda kungana na watu waliokuwa kwenye msiba huo na kukaa chini. Kila kitu kwake hakikuwa kizuri tena.

Mazishi yalipomalizika, jamaa aliendelea kuukumbuka mkasa uliomtokea, kwani alimpenda sana msichana yule licha ya kwamba alikuwa ameonana naye mara ya kwanza tu. Akajiona kama ni mtu aliyekuwa na mkosi.

Mtu ambaye aliahidiana naye, lakini akafariki siku ile ile usiku, aliona kama ni mmoja kati ya mkosi mkubwa kuupata kwenye maisha yake.

Tukio hili la kweli kabisa, likatungiwa wimbo ambao ukaitwa 'Mawazo.' Mashairi ya wimbo huo ni kama ifuatavyo.

*"Nilitembea jijini Dar es Salama nikakutana na binti mmoja, nikamweleza ninavyompenda, na yeye akasema amekubali, kesho yake akanipa ahadi, niende kwake nikamtembelee.*

*Kesho yake niliamka mapema ili nipate kuwahi ile ahadi yangu, asije kwamba akanielewa, pengine mimi nina ahadi za kiswahili.*

*Nilipofika nyumbani kwake ee ee, niliyakuta makundi ya watu jamani ee ee,wakaniambia ati alifariki usiku wa jana kuamkia leo, mawazo ooo, mawazo ooo jamani eee. Mawazo ooo, mawazo ooo, mawazo ooo, mawazo oo.*

*Kila nikilala ni mawazo ooo, hata nikitembea ni mawazo ooo, nafikiria sijui nifanye nini ili nikurudishe hapa duniani mawazo, mawazoo jamani eee.*

*Mawazo ooo, mawazo ooo, mawazo ooo, mawazo oo."* *Wimbo huu ulitamba sana kuanzia miaka ya 1980 mwanzoni hadi katikati. Hii ndiyo dunia. Dunia ni ile ile. Waendao ni viumbe.*

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

# Nyuma ya Pazia-17

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanamume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo, Dar es salaam, ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili, ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

TAYARI kulikuwa na watu watatu ambao walikuwa wamezirai kwa poda ya sumu. Alitoa kichupa cha dawa ya kuzuia damu akamwagia miguuni jamaa ili isiendelee kuvuja na kusababisha kupoteza maisha. Wote watatu aliwahitaji wazima. Na ndiyo maana hakuwaua, wala kuwapa majeraha makubwa kwa sababu bado alikuwa na kazi nao.

Aliingiza mfukoni na kutoa simu ya mkononi akampigia Kamanda wa Polisi Kanda Maalum.

"Habari afande." "Nzuri kijana, vipi mbona usiku huu?" "Ndiyo kamanda, ile kazi ambayo uliongea na bosi wangu nimeifanya tayari. Sasa kinachotakiwa ni kutuma askari wako maeneo ya Mikwambe hapa Kigamboni, barabara ya kutoka Kigamboni kwenda Tuangoma. Maeneo hayo kinajengwa kiwanda cha saruji. Kuna watu watatu ambao wanatakiwa kuchukuliwa na kwenda kuhifadhiwa. Nadhani hawa ndiyo watatusaidia kufahamu kila kitu kuhusu ile inshu ya kutekwa mtoto." "Okay, wako kwenye hali gani?" "Wamezirai wote watatu, mmoja amekimbia, waliobaki eneo hilo hilo, lakini sehemu tofauti. Nitakuandikia meseji ili wanaokuja wasipotee na wawapate kwa urahisi. Mimi nimemaliza naondoka, sitakuwepo tena eneo la tukio."

"Vizuri, lakini mimi nadhani suala hili ungemaliza mwenyewe, na tulichohitaji ni kukusanya ushahidi tu kwa ajili ya kuwapeleka mahakamani."

"Ni kweli kamanda, lakini bado. Suala halijaisha kabisa. Hatujajua nani yupo nyuma ya hili, mtoto hajapatikana, wala hatujui nani alikuwa anavujisha siri. Haya mambo matatu yote ndiyo yanayotakiwa kujulikana, sijakamilisha ila niko katika hatua ya mwisho. Ila ninachoomba hao watu wawekeni selo, wakizinduka kesho jioni msiwahoji chochote. Kuna vijana wangu nitawatuma waje kuwachukua kwa ajili ya mahojiano.

Baada ya kuongea na kamanda alichofanya ni kwenda kwenye gari ambalo lilikuwa limechakazwa kwa risasi kuanzia kwenye matairi hadi vioo. Akafungua mlango na kuchukua mkoba wa pesa ulioletwa na Macky, na kuchukuwa na waliokuja kuzichukua.

Pesa zake shilingi milioni tano na vipande vya maboksi alivyovipanga kama pesa na kumwaminisha Macky na watekaji kama zilikuwa shilingi milioni 15, vyote vilikuwa mikononi mwake tena.



**"Ni kweli tumepokea watu watatu hapa. Na tumeelezwa kuwa hawa ndiyo wale ambao walikuwa wanasumbua kipindi kile ambacho tulikuwa**

***************************************

Ilikuwa ni saa tano asubuhi. Aliamka na kwenda kuoga. Aliporudi aliandaa chai yake, akikaanga mayai matatu na mikate iliyokuwa kabatini akafungua kinywa.

Alitoka nyumbani kwake Victoria kwenda ofisini kwake Mikocheni, Dar es Salaam. Alikuwa ndani ya gari yake ndogo nyeupe aina Volvo XC90, alianza kukumbuka yaliyotokea jana.

Aliondoka eneo la tukio, kwa kutotaka mtu yeyote kujua kama yeye ndiye anashughulikia sakata hilo.

Alikuwa na uwezo wa kuwasubiri na kuwaonesha kila kitu kilichopo na alichokifanya. Lakini hakutaka. Alichofanya aliandika meseji ambayo ingeweza kuwaonesha kila kitu. Na kweli walipofika walikuta mazingira yapo kama yalivyoainishwa. Kuwapo kwa gari. Watu wawili walioonekana kama wamekufa na mwingine alionekana baadaye, eneo la mbali kidogo akivuka barabara. Huyu ndiye yule aliyekuwa wa kwanza kuvutishwa au kupewa sumu ya poda, inayomfanya mtu azimie badala ya kufa.

Mwenyewe aliondoka kabisa eneo la tukio na kuanza kutembea taratibu kando ya barabara akitoka maeneo hayo ya Mikwambe, kwenda Kongowe kupitia Tuangoma. Ni umbali mrefu. Itakumbukwa hakwenda na usafiri wake. Alikuja kwa usafiri wa daladala. Muda huo ulikuwa ni saa nane usiku hivyo hakukuwa na usafiri wowote. Hivyo alitembea kando ya barabara ili kuvuta muda kuanze kupambazuka ili apate usafiri. Haikuwa rahisi sana. Alifika Tuangoma na alipokuwa karibu kufika Kongowe ndipo kulipopambazuka, bodaboda na magari mengine yakaanza kupita.

Alikodi bodaboda hadi Mbagala, akapanda mabasi ya kwenda Mwenge kupitia Kinondoni Morocco. Alishuka kwenye kituo cha Victoria saa moja asubuhi. Hakipo mbali sana na nyumbani kwake. Akakumbuka pia kazi aliyoifanya ambayo sasa itakwenda kukamilika na kumaliza kitendawili chote.

Alipofika ofisini alimpigia Mkuu wa Kituo cha Polisi Kinondoni, kuulizia kama tayari wameshafanikisha.

"Ni kweli tumepokea watu watatu hapa. Na tumeelezwa kuwa hawa ndiyo wale ambao walikuwa wanasumbua kipindi kile ambacho tulikuwa tunawawekea mtego wa kuwakamata."

"Okay kamanda sasa muda si mrefu tutajua yote, ni kiasi cha kuvuta subira, si hawajaamka bado?" "Bado, bado wamezirai hawa." "Okay, tunasubiri hilo." "Ahsante kamanda." Alisema Eddy na kukata simu.

Simu ya pili alimpigia Macky. "We bwana nakuhitaji ofisini. Chukua bodaboda haraka uje."

"Vipi una taarifa yoyote ya kuachiwa kwa mtoto?" Akauliza Macky kwenye simu.

"Mambo ya mtoto tutakuja kuyazungumza huku sio kwenye simu braza." Akajibu Eddy.

**********************************

"Unajua mimi hapa nimeshachanganyikiwa kabisa!" Macky hakuwa na haja ya kumwambia hivyo Eddy, kwani alionekana kabisa hakuwa sawa.

"Hebu kaa kwanza kwenye kiti." Eddy alimpoza, kwani alipoingia tu alianza kuuliza maswali badala ya kusalimia. Macho yalionekana kumtoka pima kama mtu aliyetoka kuokoka kwenye kifo.

"Ndugu mwandishi, inakuwaje pesa tumeshawapa, lakini hawajanipigia tena simu kwa ajili ya kumwachia mtoto wangu Macaire?" "Kwani mara ya mwisho wakati walipokwambia ukaweke pesa walikwambia utampataje?" "Walisema wakizipata tu pesa kesho yake asubuhi, saa tatu au nne watanipigia simu sehemu ya kwenda kumchukua. Tena waliniambia mtoto yupo salama tu. Nashangaa pesa ulizonipa ndugu mwandishi nimekwenda kuziweka sehemu ile ile ambayo walisema, lakini hadi saa tano sijapokea simu yoyote." "Ina maana wametutapeli?" Eddy akauliza.

"Ndiyo inavyoonekana, pesa shilingi milioni 15 wamechukua na mtoto hawataki kumuachia, imenizunisha sana." Akasema Macky akionekana kuchoka mwili na akili pia.

"Ni kweli ulipeleka pesa sehemu sahihi na zilikuwa kamili?" "Ndiyo kila kitu nilifanya sahihi."

"Sasa kwa nini hawajapiga simu ya kumwachia mtoto? "Sijui?" Tabasamu la Eddy lilikuwa ndani ya moyo wake. Hakutaka kulionyesha. Kitu ambacho Macky hakufahamu ni kwamba Eddy alikuwa eneo la tukio na alimuona akiwa na mkoba akivuka barabara na kwenda kuweka pesa. Na yeye ndiye alikuwa anamlinda ili asipate madhara kutoka kwa watekaji kama wangetaka kumdhuru. Hakufahamu kama baada ya yeye kuweka pesa na kuondoka, wachukua pesa walikipata cha moto kutoka kwa Eddy, ambaye yeye anamfahamu kama mwandishi wa habari. Na ndiye aliyemkopesha pesa. Hakujua kuwa mkoba wa pesa aliopewa ili akawape watekaji wa mtoto, umerudi tena mikononi mwake. "Au hawakuja tena kuchukua pesa, kuna mtu ametoa siri kwao?" "Sidhani, kwa sababu safari hii sikupigiwa simu yoyote ya kuniambia rudi na mkoba wako. Safari hii hawakunipigia simu kunishutumu au kunitisha kuwa tumewaambia askari polisi waje eneo la tukio ili waende kuwakamata. Kwa maana hiyo inaonekana wameupata. na huu ukimya, inaonekana kweli mzigo wameuchukua. Isingekuwa hivyo wangekuwa wameshanipigia kama ilivyo mara zote wanavyofanya."

**Itaendelea Jumapili**



# NAFASI ART SPACE WATOA FURSA WASANII WA KIKE

**Na Judith Julius**

KITUO cha kuendeleza sanaa kilichopo jijini Dar es Salaam, kiitwacho Nafasi Art Space, kikishirikiana na taasisi ya WeWorld, kimetoa fursa kwa wasanii wa kike kujiunga na mradi wa wasichana katika haki ya hedhi.

Taarifa iliyotolewa na uongozi wa Nafasi Art Space imebainisha kuwa wasanii hao watajikita katika sanaa ya uchoraji, wabunifu wa vielelezo, na ushonaji.

Wasanii watakaochaguliwa kujiunga na mradi huo watapata nafasi ya kujiunga na kundi mahiri la wasanii wabunifu.

Kituo hicho kimewasihi wasanii wa kike wasiipoteze fursa hiyo ya kuleta mabadiliko kupitia sanaa.



# MUNGU INUSURU HOLLYWOOD

HALI imekuwa ya majozi nchini Marekani, baada ya moto mkali kuendelea kuteketeza eneo maarufu zaidi na kivutio la Los Angeles katika California.

Sasa eneo linalojulikana kuishi mastaa wa filamu la HollyWood, linawaka moto na tayari mlima ambao unatambulika kama Hollywood Hills umeungua.

Eneo hilo ambalo linajulikana duniani kama utambulisho wa Sanaa ya filamu nchini Marekani, limebaki kuwa majivu baada ya moto huo kuteketeza nyumba za waigizaji na ukumbi maarufu wa HollyWood.

Juhudi za kuuzima moto huo zinaonekana kushindikana kutokana na upepo mkali kuusaidia kusambaa kwa kasi.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MALEN APANDISHWA DAU

KLABU ya Aston Villa imeongeza dau la kumnunua mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Donyell Malen, hadi kufikia euro milioni 25, lakini timu hiyo ya Ujerumani bado inadai euro milioni 30 kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi mwenye umri wa miaka 25. (**Florian Plettenberg**)

### GOMES AGOMBEWA ENGLAND

MANCHESTER United, Arsenal na Liverpool zinamtaka kiungo wa kati wa Wolves na Timu ya Taifa ya Brazil mwenye umri wa miaka 23, Joao Gomes. (**Sun**)

### MONACO YAMTAKA RASHFORD

MONACO ni klabu ya hivi karibuni kuonyesha nia ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester United mwenye umri wa miaka 27, ambaye ni raia wa England, Marcus Rashford. (**Telegraph**)

### DURAN AKARIBIA PSG

KLABU ya Paris St-Germain inamtaka mshambuliaji wa Aston Villa mwenye umri wa miaka 21, raia wa Colombia, Jhon Duran. (**RMC Sport**)

### MUANI ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United inafanya kila liwezekanalo kuipiku Tottenham Hotspur katika usajili wa mshambuliaji wa Paris St-Germain, raia wa Ufaransa, Randal Kolo Muani, mwenye umri wa miaka 26. (**Team Talk**)

### ELLIOT SOKONI ULAYA

KLABU ya Brighton na Borussia Dortmund inavutiwa na winga wa Liverpool mwenye umri wa miaka 21, Harvey Elliott. (**Sun**)

### NEMANJA ATAKIWA IPSWICH

KLABU ya Ipswich inachunguza mpango wa kumsajili kiungo wa zamani wa Serbia, Nemanja Matic, mwenye umri wa miaka 36 ambaye kwa sasa anaitumikia Lyon. (**Florian Plettenberg**)

### BILLINGI KUTUA NAPOLI

KIUNGO wa kati wa Bournemouth na Timu ya Taifa ya Denmark, Philip Billing, amesafiri kwa ndege hadi Italia kukamilisha uhamisho wa mkopo kwenda Napoli. (**Fabrizio Romano**)

### NUAMAH ATAJWA EVERTON

KLABU ya Everton inafikiria kuwasilisha ombi la kumnunua winga wa Lyon raia wa Ghana, Ernest Nuamah, mwenye umri wa miaka 21. (**RMC Sport**)

### COULIBALY MAMBO SAFI

LEICESTER City imekubali dili la kumsajili beki wa pembeni wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Woyo Coulibaly, mwenye umri wa miaka 25 kutoka Parma. (**Gianluca di Marzio**)

### CARLOS NJIA MOJA

KLABU ya Fenerbahce imefanya mazungumzo na Aston Villa kuhusu mkataba wa pauni milioni 10 kwa beki wao wa kati Mbrazil, Diego Carlos, mwenye umri wa miaka 31. (**Sky Sports**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# LEWANDOWSKI: BARCA INATAKIWA IJIBORESHE

**JEDDAH,** Saudi Arabia

**Mshambuliaji huyo asema ndio njia pekee itakayowasaidia kushinda...**

MSHAMBULIAJI wa Barcelona, Robert Lewandowski, amesema timu hiyo bado inahitaji kuboresha mitazamo yake ili kushinda mataji makubwa msimu huu wakati wanapojiandaa na mechi ya fainali ya Supercopa dhidi ya Real Madrid itakayochezwa leo.

Barca iliichapa Madrid mabao 4-0 mwanzoni mwa msimu wa LaLiga na kushinda mechi 11 kati ya 12 za mwanzo, lakini wameshinda mchezo mmoja tu kati ya saba iliyofuata kwenye ligi, na kushuka hadi nafasi ya tatu katika msimamo.

Vijana hao wa Kocha, Hansi Flick, wamepoteza kwa Las Palmas na Leganés wakiwa nyumbani, huku Lewandowski akikubali wamepoteza pointi katika michezo ambayo walistahili kushinda.

**"Ni mapema mno kusema kama tunaweza kushinda kitu," alisema mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland akiiambia ESPN kutoka kituo cha Barca huko Jeddah.**

"Bila shaka, tunaweza kushinda kila mtu. Lakini ili kushinda kila kitu, unahitaji bahati wakati wa msimu pia. Tuna uwezo wa ajabu, lakini uwezo ni kitu kimoja na mtazamo ni jambo la pili.

"Tunathibitisha mengi. Tunathibitisha sana mawazo yetu. Lakini, kwa mfano, kama unataka kushinda ligi, lazima ushinde michezo midogo.

"Tumepoteza pointi na ... sitaki kusema michezo midogo, lakini michezo ambayo kwetu tulistahili kushinda.

"Natumaini mwaka huu pia tutashinda michezo hii ambayo tunapaswa kushinda na pia michezo mikubwa. Hiyo ni hatua inayofuata kwa wachezaji wachanga, kwetu, kwa kila mtu kuimarika."

Lewandowski pia anatumanii kudorora kwa Barca kabla ya Krismasi kulikuwa njia ya kujifunza kwa kipindi cha pili cha msimu.

# ARSENAL YAKWAA KISIKI KUPATA HUDUMA YA ISAK



**LONDON,** England

BEI iliyowekwa na Newcastle United ya pauni milioni 150 ili kumwachia mshambuliaji wake, Alexander Isak, inatarajiwa kuwa kikwazo kwa Arsenal kuipata saini ya mchezaji huyo, kwa mujibu wa ESPN.

Kocha wa Arsenal, Mikel Arteta, amekuwa akimwania Isak kwa muda mrefu na alifunga bao lake la 15 katika michuano yote msimu huu wakati Newcastle ilipoondoka Emirates ikiwa na ushindi wa mabao 2-0 katika mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Kombe la Carabao katikati ya wiki.

Kwa kufahamu ubora wa Isak, Newcastle imetoa changamoto kwa pande zote zinazohitaji kuvunja rekodi ya uhamisho ya Uingereza ili kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, raia wa Sweden, ambaye thamani yake ni pauni milioni 150.

Gazeti la Daily Mail limeripoti mmiliki wa Arsenal, Stan Kroenke, hana uwezekano wa kutoa kiasi hicho cha fedha kumnunua Isak, hivyo amempa changamoto Arteta kutafuta mlengwa mbadala na wa bei nafuu.

Arsenal haiaminiki iko katika hatari ya kukiuka kanuni za fedha za Ligi Kuu England, lakini kuna hofu matumizi makubwa kama hayo kwa mchezaji mmoja yanaweza kuathiri vibaya uwezekano wao wa kubakia ndani ya kanuni.

Mshambuliaji, Gabriel Jesus atapatikana kwa uhamisho msimu wa joto, huku mlinzi, Oleksandr Zinchenko, akielekea nje ya mlango mapema zaidi.

Newcastle wanataka kumbakisha Isak, ambaye amesisitiza hadharani furaha yake huko St James' Park, lakini Magpies hawawezi kushindana na fedha zinazopatikana katika klabu kubwa.

# Man City yafanikiwa kumsajili Khusanov

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City iko katika hatua nzuri ya kuinasa saini ya beki Abdukodir Khusanov baada ya kufikia makubaliano na Lens kwa ajili ya uhamisho wake, vyanzo vimeiambia ESPN.

City wanakaribia kukamilisha dili la zaidi ya pauni milioni 40 kwa beki huyo wa kati wa Uzbekistan mwenye umri wa miaka 20.

Wawakilishi wake wako jijini Manchester kujadili maelezo ya mwisho na uchunguzi wa kimatibabu unaweza kufanyika wiki hii kabla ya tangazo rasmi.

Ikiwa kila kitu kitaenda sawa, Khusanov atakuwa mchezaji wa kwanza kusajiliwa na City katika dirisha la usajili la Januari.

Khusanov anatazamiwa kujiunga na kikosi cha kwanza cha Pep Guardiola mara moja ili kufukia mapengo ya Rúben Dias na John Stones ambao ni majeruhi.

Guardiola ameachwa bila mabeki wa kati msimu huu huku Manuel Akanji na Nathan Aké wakiwa nje ya uwanja.

Lens inatazamiwa kupata faida kubwa kutokana na uhamisho huo wa Khusanov kwenda Ligi Kuu England.

Beki huyo alijiunga na klabu hiyo ya Ligue 1 akitokea Energetik-BGU katika ligi kuu ya Belarus Julai 2023 kwa mkataba wa thamani ya Euro 100,000 na sasa yuko tayari kuhamia City kwa fedha nyingi akiwa ameichezea klabu hiyo ya Ufaransa mechi 31.

Vyanzo viliiambia ESPN, Lens ilitaka kumbakisha beki huyo kwa miezi sita zaidi, lakini ilibidi wakubaliane kusawazisha vitabu vyao baada ya kukosa zaidi ya euro milioni 40 katika ada ya uhamisho msimu uliopita wa joto wakati uhamisho wa Kevin Danso na Neil El Aynaoui.

Vyanzo vilisema klabu hiyo ilimwomba wakala Jorge Mendes kumtafutia Khusanov klabu mpya mwezi huu.



# Vinicius Jr kununua klabu Ureno

**MADRID,** Hispania

NYOTA wa Real Madrid, Vinicius Junior, anafikiria kuinunua klabu ya soka ya daraja la pili iliyoko Ureno, kwa mujibu wa ESPN.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil, kwa sasa yuko Jeddah, Saudi Arabia, kwa ajili ya fainali ya michuano ya Supercopa ya Hispania, na anafikiria juu ya kubadilisha masilahi yake ya kibiashara kwa kuangalia mipango yake ya baadaye ya kazi baada ya kustaafu kama mchezaji.

Vinícius alianza katika kikosi cha Madrid kilichopata ushindi wao wa 3-0 wa nusu fainali ya Supercopa dhidi ya Mallorca hapo juzi, matokeo ambayo yatawafanya wakabiliane na Barcelona kwenye fainali itakayochezwa leo.

Habari za mshindi wa pili wa Ballon d'Or kufikiria kununua klabu ziliripotiwa kwa mara ya kwanza na kituo cha redio cha Cadena COPE.



Vinícius tayari ana mfululizo wa mikataba ya udhamini binafsi, pamoja na mkataba na Nike ambao utaendelea hadi mwaka 2028.

Vinícius na Nike hivi karibuni walifikia makubaliano mapya baada ya mzozo wa kisheria, ambao unamfanya Mbrazil huyo kuwa mmoja wa watu mashuhuri wa kampuni hiyo ya Marekani katika soka.

Vinícius anawakilishwa na wakala wake, Roc Nation, na anawasiliana mara kwa mara na wanamichezo mashuhuri kutoka michezo mingine, haswa NBA na NFL.

Pia anakuza msingi wa hisani wa Taasisi ya Vini Jr ya Brazil.

Ligi Daraja la Pili la Ureno linashirikisha timu 18, zikiwamo timu za akiba za Benfica na Porto. Klabu moja, Portimonense, tayari ina Mbrazil kwenye usukani, Rodiney Sampaio.

Vinícius hatakuwa mwanasoka wa kwanza ambaye anaendelea kucheza kununua klabu.

N'Golo Kanté anamiliki Royal Excelsior Virton iliyoko Ligi Daraja la Tatu nchini Ubelgiji, na Kylian Mbappé, ana hisa kubwa ndani ya Caen iliyopo Daraja la Pili huko Ufaransa.

HABARI MICHEZO

# MAKIPA 12 LIGI KUU BARA WASOTEA BENCHI 2024/25

**Na Adam Fungamwangwo**

JUMLA ya magolikipa 12 wanaocheza katika timu za Ligi Kuu Tanzania Bara hawajadaka mechi hata moja hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo, imefahamika.

Simba inaongoza kuwa na idadi kubwa ya makipa wake kati ya wanne iliyowasajili hawajasimama langoni hata mchezo mmoja, ikifuatiwa na Kagera Sugar ambayo makipa wake watatu hawajawahi kukaa golini.

Kwa mujibu wa rekodi zetu na za Bodi ya Ligi, makipa hao ni wale waliosajiliwa kuzichezea timu 16 za Ligi Kuu Tanzania Bara ambazo zinapambana kuwania ubingwa unaoshikiliwa na Yanga.

Makipa wa Simba ambao hawajaonja ladha ya kukaa langoni tangu msimu uanze ni Ayoub Lakred raia wa Morocco, Aishi Manula 'Tanzania One', Hussein Abel na Ally Salim.

Kwa upande wa Kagera Sugar, makipa watatu ambao wamekaa benchi mzunguko wote wa kwanza, ni Shija Jackson, Bruno Bruno na Said Kipao.

Katika michezo yote 15 ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyocheza, Simba imemsimamisha langoni, Moussa Camara, ambaye ni raia na Guinea, huku Kagera Sugar ikimtumia Ramadhani Chalamanda katika michezo yote.

Makipa wa Azam FC, ambao mpaka sasa bado hawajakaa langoni ni Ali Ahmada na Hamisi Athumani.

Makipa wengine ambao wamesugua benchi bila kucheza walau dakika moja ni Ibrahim Parapada wa Singida Black Stars, Lameck Kanyonga wa Mashujaa FC, na Shaaban Kimwaga wa KMC.

Wakato huo huo, kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum, anaongoza kuchangia, mabao mengi katika ligi hiyo ambayo itaendelea tena ifikapo Machi Mosi, mwaka huu.

Fei Toto amechangia jumla ya mabao 13 mpaka sasa kwenye timu yake, akifunga manne na kutoa pasi za mwisho tisa.

Anafuatiwa na kiungo mshambuliaji wa Simba, Jean Ahoua, ambaye amechangia mabao 12 katika timu yake, akitoa 'asisti' tano na kufunga mabao saba mpaka sasa.

Clement Mzize, Pacome Zouzoua wote kutoka Yanga, na Elis Rupia wa Singida Black Stars wamechangia mabao tisa kwenye timu zao kila mmoja.

Mzize amefunga mabao sita na 'asisti' tatu, Pacome amepachika mabao matano akiwa na 'asisti' nne, huku Rupia anayeongoza kwenye mfungaji kwenye Ligi Kuu na mabao yake manane, ana 'asisti' moja.




Kipa wa City Lights kutoka Sudan Kusini, Caesarina Moses (kushoto), akidaka mpira na kuokoa shambulizi la nyota wa Kenya Academy Sports, Precious Kimtai (kulia), katika mechi ya Mashindano ya Wasichana ya CAF U-17 (GIFT), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi jioni. Timu ya Kenya ilipata ushindi wa mabao 5-1. **PICHA: TFF**

# Yanga Princess yaimarisha ulinzi

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inaanza mzunguko wa pili wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania ikiwa imara, uongozi wa Yanga Princess umetangaza kumsajili aliyekuwa beki wa kati wa Fountain Gate Princess, Protasia Mbunda.

Beki huyo wa zamani wa timu ya taifa ya wanawake (Twiga Stars), tayari ameshaanza mazoezi na timu yake mpya inayofundishwa na Kocha Mkuu, Edna Lema.

"Ni kweli tumeshakamilisha taratibu za kumnasa Protasia, tunaamini atakuwa msaada mkubwa katika kikosi chetu kuelekea hatua ya lala salama ya ligi, tunataka kujenga kikosi chenye ushindani zaidi," kilisema chanzo chetu.

Chanzo hicho kiliongeza tayari kikosi chao kimeshaanza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi za ligi ambayo itarejea tena kuanzia Januari 22, mwaka huu.

Katika msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, Yanga Princess yenye pointi 12 iko kwenye nafasi ya nne nyuma ya vinara, Simba Queens yenye pointi 25 ikifuatiwa na JKT Queens yenye pointi 20 lakini ikicheza mechi moja pungufu.

Mashujaa Queens yenye pointi 15 iko katika nafasi ya tatu wakati Mlandizi Queens ya Mlandizi mkoani, Pwani inaburuza mkia ikiwa na pointi moja.

Ligi hiyo ilisimama kupisha maandalizi ya Timu ya Taifa ya umri chini ya miaka 17 (Serengeti Girls), ambayo ilikuwa inakabiliwa na mechi ya kufuzu Fainali za Kombe la Dunia dhidi ya Eswatini, ambayo imejitoa katika michuano hiyo na hivyo Tanzania imesonga mbele.

# Momade asajiliwa kuinusuru Prisons

**Na Adam Fungamwangwo**

BAADA ya kumsajili straika, Kelvin Sabato 'Kiduku', Prisons imeendelea kukiboresha kikosi chake kuelekea katika mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, baada ya kupata saini ya kiungo mshambuliaji, raia wa Msumbuji, Amade Momade.

Mkataba huo umesainiwa katika Ofisi za Michezo Makao Makuu ya Magereza jijini, Dodoma na kushuhudiwa na Mkuu wa Kitengo cha Michezo Jeshi la Magereza SSP, Erasto Jackson Ntabahanyi na Msaidizi wake SSP, Bakari Hamisi Sudi.

Ntabahanyi aliliambia gazeti hili usajili huo umezingatia mahitaji na ushauri uliotolewa na Kocha Mkuu Prisons, Amani Josiah, ambaye amechukua mikoba ya Mbwana Makata, aliyeonyeshewa mlango wa kwaheri hivi karibuni.

Bosi huyo alisema mchezaji hyyo mpya alisaini mkataba wa mkopo na Prisons baada ya kufikia makubaliano na viongozi wake wa Singida Black Stars.

"Tumefanikiwa kumnasa Amade, ambaye atakuwa na sisi hadi mwishoni mwa msimu. Kabla ya kutua kwetu, alikuwa ni mchezaji wa mkopo wa klabu ya Namungo," ilisema taarifa rasmi iliyotolewa na Prisons.

Taarifa iliwataja wachezaji wengine ambao wamesajiliwa na timu hiyo ni pamoja na Rabbin Sanga na Athuman Sufian Mwemfua.

Usajili huo ni mkakati maalum kuhakikisha Prisons inafanya vyema katika mzunguko wa lala salama wa Ligi Kuu, baada ya kushindwa kuonyesha makali yake kwenye mzunguko wa kwanza.

Hadi kumalizika kwa mzunguko wa kwanza, Prisons iko katika nafasi ya 13 ikiwa na pointi 14 baada ya kucheza michezo 16, ikishinda michezo mitatu, sare tano na imepoteza michezi nane.

Klabu mbalimbali zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara, Ligi Kuu ya Wanawake Nchini zinaendelea kujiimarisha huku zikiwa zimebaki siku tatu ili kufungwa na dirisha dogo la usajili.

Ligi hiyo ilisimama kupisha mashindano ya Kombe la Mapinduzi, mechi za michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika pamoja na Fainali za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).




Lewandowski: Barca inatakiwa ijiboreshe UK. 21


# Simba, Yanga ni zaidi ya vita CAF

## Vigogo hao wanahitaji ushindi ili kuwasha 'taa za kijani' kuelekea...

**Na Adam Fungamwango**

USIKU wa deni haukawii, wawakilishi wa Tanzania waliobakia katika mashindano ya kimataifa, Simba na Yanga zitashuka katika viwanja viwili tofauti ugenini leo ili kucheza mechi zitakazoamua hatima ya nafasi yao ya kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wao watawavaa Al Hilal katika mechi ya Kundi A ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa kuanzia saa 4:00 usiku kwenye Uwanja wa De la Capitale nchini, Mauritania huku Bravos do Maquis ya Angola ikiwakaribisha Simba kwenye mchezo wa Kombe la Shirikisho kuanzia saa 1:00 usiku.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, alisema amekiandaa vyema kikosi chake kwa ajili ya kupambana bila kumwangalia mpinzani anacheza vipi.**

Kocha wa Yanga, Ramovic, amesema tayari amekiandaa kikosi chake kwa ajili ya mchezo huo, akitarajia kupata matokeo mazuri licha ya ubora wa wapinzani wao.

"Kikosi kiko tayari, nimekiandaa kwa ajili ya kucheza mechi, simwangalii mpinzani ili kuwa bora, napambana kuhakikisha nashinda mchezo, ninachokifurahia zaidi ni namna timu yangu inavyoimarika na ipo kwenye morali nzuri, hivyo naamini kila kitu kinawezekana kwa kushindana," alisema kocha huyo.



Ramovic - Yanga SC | Fadlu - Simba SC

Meneja wa Yanga, Walter Harrison, alisema katika mchezo wa leo kikosi chao kimepata na mashabiki wengi, ambao wameahidi kwenda kuwashangilia uwanjani kwa sababu baadhi ya wachezaji wanatoka nchi za Afrika Magharibi.

"Tumepata sapoti ya baadhi ya mashabiki kwa sababu baadhi ya nyota wetu wanatokea kwenye ukanda huu wa Afrika Magharibi, Djigui Diarra huku ni maarufu sana na amekuwa na wapenzi wengi hapa, hasa ikizingatiwa hizi nchi ni majirani, yaani amekuwa ndiyo kama mwenyeji wetu. Stephane Aziz Ki na Pacome Zouzoua nao wamekuwa kivutio kikubwa sana, imetufanya tuwe na mashabiki wengi na leo watakuwa uwanjani kutushangilia, tutakuwa kama tupo nyumbani tu," alisema Harrison.

Ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele katika mashindano hayo, Yanga inapaswa kushinda mchezo huo na hii imekolezwa na mpinzani wake mkubwa, MC Alger ya Algeria kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DR Congo).

Matokeo hayo yamewafanya MC Alger kufikisha pointi nane, hivyo Yanga itakuwa ikisaka ushindi kwa udi na uvumba ili kufikisha pointi saba, lakini pia ikihitajika kushinda mchezo wake wa mwisho dhidi ya Waarabu hao hapa nyumbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Naye Kocha Mkuu wa Al Hilal, Florent Ibenge, ambaye timu yake imeshafuzu hatua inayofuata, alisema anaweza kubadili kikosi chake katika mechi ya leo na kupanga baadhi ya wachezaji ambao hawakupata nafasi kwenye michezo iliyopita kwa ajili ya kulinda nguvu kuelekea hatua ya robo fainali.

"Kwa sasa tunayo nafasi ya kupumzika kidogo na kujiandaa kwa hatua inayofuata. Hatuwezi kupuuza umakini, lakini ni muhimu pia kuhakikisha wachezaji wangu wanakuwa na nguvu za kutosha kwa changamoto kubwa zilizo mbele yetu.

Mchezo dhidi ya Yanga utakuwa na umuhimu mkubwa kwao, lakini kwa upande wetu, tunahitaji kujiandaa kwa hali yoyote. Siwezi kujivunia mapema. Wachezaji wangu watahitaji kupumzika kidogo kabla ya michezo inayofuata," alisema kocha huyo.

Wakati huo huo, Kocha Mkuu wa Simba, Fadlu Davids, ameweka wazi wataingia uwanjani kwa ajili ya kusaka ushindi na si sare kwa sababu timu kubwa kama yake haiwezi kujiandaa kugawana pointi na mpinzani.

"Tunahitaji sare kufuzu, na ushindi ili kuongoza kundi. Sisi siyo timu ya kucheza kusaka sare, tutajitahidi kushinda mechi. Lakini tunahitaji walau sare na ushindi mmoja katika mechi zetu mbili zilizobaki au kushinda zote.

Tunapaswa kuwa makini sana, Bravos wanacheza mechi kwa fujo, yaani kushambulia zaidi. Nadhani tunapaswa kucheza tofauti na wanavyopenda wao, tucheze tofauti na tulivyocheza mechi ya CS Sfaxien. Tunapaswa kuitawala mechi zaidi, tukiwa na mpira na bila mpira," alisema Fadlu.

Kocha huyo alisema kitu ambacho kitakuwa faida kwao ni hali ya hewa ya Luanda ambayo haitofautiani na ile iliyoko Dar es Salaam.

"Tunafurahi tumepata mapokezi mazuri kutoka kwa watu wa Angola, timu ipo katika hali nzuri. Hali ya hewa ni kama Dar es Salaam, tupo tayari kwa mchezo," Fadlu alisema.

Kiungo wa Wekundu wa Msimbazi, Debora Fernandes, ambaye ni raia wa nchi hiyo, amesema mchezo huo utakuwa mgumu kwa sababu anafahamu ubora wa Bravos do Maquis inapokuwa nyumbani, lakini hiyo haiwezi kuwafanya wasitimize malengo yao.

"Utakuwa mchezo mgumu, natambua wanacheza nyumbani na wanahitaji pointi tatu, ila malengo ya Simba yanajulikana, ni kuhakikisha tunafanya vizuri," kiungo huyo alisema.

Mario Soares, Kocha Mkuu wa Bravos do Maquis, ameliambia gazeti hili mechi hiyo itakuwa nzuri na ngumu, huku akisema wanakwenda kucheza na timu yenye wachezaji wazuri na wenye uwezo wa kumaliza mechi, huku akimhofia zaidi, Jean Ahoua.

"Ina wachezaji wazuri, ni ngumu kumtaja kila mmoja kwa jina, ila mmoja wao ni yule mwenye jezi namba 10, kwangu huyo ndiyo hatari zaidi, anacheza taratibu tu, lakini mipira yake ni hatari sana," alisema kocha huyo.

Simba inahitaji sare tu katika mchezo wa leo ili kufuzu hatua ya robo fainali kutoka Kundi A, kwa sababu itafikisha pointi 10 ambazo hata kama Bravo do Maquis watafikisha kwa kushinda mchezo wa mwisho dhidi ya CS Sfaxien ya Tunisia na Wekundu wa Msimbazi wakapoteza dhidi ya CS Constantine, bado watakuwa wamefuzu kutokana na matokeo ya walivyokutana wenyewe kwa wenyewe. Ikumbukwe katika mchezo wa kwanza ulichezwa Novemba 7, mwaka jana hapa nyumbani Mnyama alipata ushindi wa bao 1-0.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >